EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

HUDUMA ZA KIJAMII NA UHAMISHAJI WA WATU NA MAKAZI KWA AJILI YA UJENZI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI, SEHEMU YA TANZANIA

MPANGO KAZI WA UHAMISHAJI WA WATU NA MAKAZI KATIKA MAENEO YA KIPAUMBELE

TOTAL EAST AFRICA MIDSTREAM BV

MARCH 2019



TOTAL TULLOW UNOC

RAP Contractors

Whiteknights DIGBY WELLS ENVIRONMENTAL

MUHTASARI WA UTENDAJI

1. UTANGULIZI

Taarifa hii ni Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi kwa ajili ya maeneo ya ujenzi wa awali (katika taarifa hii yanarejelewa kama Maeneo ya Kipaumbele) yanayohitajiwa kwa ajili ya sehemu ya Tanzania ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki. Sehemu ya Tanzania inayopitiwa na bomba hili ina urefu wa kilometa 1,147 ambalo litapita katika mikoa minane (8), na halmashauri 27; za wilaya, miji na majiji.

Muhtasari wa Jumla

Njia ambayo bomba litapita imechaguliwa ili kupunguza athari za kimazingira na kijamii, kuhamishwa (kupoteza makazi) na kuondolewa katika maeneo ya kiuchumi (kupoteza kabisa au kwa kiwango fulani njia ya kuingiza kipato) kwa jamii.

Utekelezaji wa Mradi huu unafuata sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuzingatia viwango vya Mradi kama vilivyoainishwa katika Makubaliano ya Ushirikiano baina ya Serikali mbili na masharti ya Taasisi za Fedha za Kimataifa (IFI). Kwa mujibu wa viwango hivi, Mfumo wa Sera za Kuwahamisha Watu umeandaliwa kwa sehemu ya Mradi ya Tanzania, na Mipango Kazi mahususi ya Kuwahamisha Watu itaandaliwa kwa ajili ya Maeneo yanayopewa Kipaumbele na kwa ajili ya kila mkoa kati ya mikoa 8 kulingana na kanuni zilizowekwa katika Mfumo wa Sera za Kuwahamisha Watu. Waraka huu ni Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu kwa Maeneo ya Kipaumbele.

Mradi utahitaji kutumia hekta 4,000 za ardhi nchini Tanzania zikijumuisha Maeneo ya Kipaumbele (~325 ha), ambazo zitarasimishwa kabla ujenzi wa bomba haujaanza.

Kusudi na Mawanda

Mpango Kazi huu wa Uhamishaji wa Watu na Makazi unafafanua sera, kanuni, taratibu, majukumu na wajibu kwa ajili ya kumudu athari za kuhamisha watu katika makazi na athari za kuondoa watu katika vyanzo vya kiuchumi yanayosababishwa na kuchukuliwa kwa ardhi kwa ajili ya Maeneo ya Kipaumbele.

Mashauriano na ushirikishaji wa jamii zilizoathirika na wenyeji unakopita Mradi na ngazi zote za uongozi wa Serikali ya Tanzania yatakuwa yakiendelea katika muda wote wa utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya uhamishaji wa watu. Lengo la jumla la Mradi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi ni kuwahamisha watu kwa namna inayotoa, kwa kaya zilizoondolewa katika makazi yao na zile zilizoondolewa katika vyanzo vyao vya kiuchumi, fursa ya kuboresha au walau kurejesha viwango vyao vya awali vya kimaisha na uingizaji wa kipato.

Mawanda ya Mpango Kazi huu wa Uhamishaji wa Watu na Makazi ni kubaini na kufafanua:

- Watu walioathiriwa na utwaaji wa ardhi katika Maeneo ya Kipaumbele ambao wataondolewa katika makazi yao na/au maeneo yao ya kiuchumi;
- Vigezo vya kustahili kwa pande zilizoathirika;
- Viwango vya ulipaji fidia kwa mali zinazopotea;

- Viwango vya msaada katika uhamishaji wa watu kwa kaya zilizoathiriwa;
- Hatua za kurejesha njia za uingizaji wa vipato kwa watu au kaya zilizoathiriwa;
- Hatua zilizochukuliwa kupunguza au kuepuka kuwaondoa watu;
- Wajibu na majukumu ya kukusanya, kushughulikia na kutekeleza hatua za Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu; na
- Shughuli zilizohitaji kuthibitishwa za Mpango Kazi huu wa Uhamishaji wa Watu ili kutekeleza na kufuatilia majukumu ya Utwaaji wa ardhi, ulipaji wa fidia na ufufuaji wa njia za kuingiza kipato ulioahidiwa humu.

2. MAELEZO YA MRADI

Mradi ni wa muundombinu wa kilomita 1,443 wa kusafirisha mafuta Ghafi ya Uganda kutoka Kabaale-Hoima nchini Uganda kwenda rasi ya Chongoleani karibu na bandari ya Tanga nchini Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta katika soko la kimataifa. Mfumo huu mkuu wa usafirishaji, (Kilomita 296 Uganda na 1,147 Tanzania), unaundwa na bomba lenye upana wa inchi 24 lililofunikwa ardhini na lenye mfumo wa kutunza joto, Vituo 6 vya kusukuma mafuta (2 nchini Uganda na 4 nchini Tanzania) na kituo cha kuhifadhi na kupakia mafuta kwa ajili ya usafirishaji katika bandari maalum.

Bomba litafukiwa kwenye kina cha urefu wa mita 1.8 – 2 chini ya ardhi. Litafukiwa chini zaidi katika maeneo litakapovuka mito na barabara.

Njia inayopendekezwa kupita bomba hilo na Maeneo ya Kipaumbele imeonyeshwa katika Kielelezo ES-1 ambacho pia kinaonyesha maeneo yaliyopendekezwa ya mitambo ya kusukuma mafuta itakayofungwa juu ya ardhi. Mitambo hii ni pamoja na: vituo vya kusukuma mafuta, vituo vya kufuatilia hali ya joto la bomba; vituo vyenye valvu kuu kwa ajili ya kuzuia/kuruhusu mafuta kupita; kituo cha kuhifadhi na kupakia mafuta kwa ajili ya usafirishaji katika bandari maalum; na vituo vya kushushia mafuta.



Kielelezo ES-1: Mahali Yalipo Maeneo ya Kipaumbele katika Mkuza wa Bomba la Mafuta Ghafi

Mafuta ghafi ya Uganda yana asili ya uzito na nta katika hali ya joto la kawaida, hivyo huganda katika hali hii. Kwahiyo, ili kusafirisha mafuta haya, Bomba la Mafuta ghafi la Afrika Mashariki litahitaji kupashwa joto kwa kiwango cha chini cha C50° na kuwekewa mfumo wa kutunza joto. Ili kudumisha hali hii ya joto, Bomba litapashwa joto kwa kutumia umeme ili kuyafanya mafuta yabaki katika hali ya kimiminika kutoka mwanzo hadi mwisho wa mkuza wa bomba. Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki litakua bomba refu zaidi duniani linalopashwa joto kwa njia ya umeme.

Bomba litakatiza nchi 2, Uganda na Tanzania. Nchini Uganda, litakua na urefu wa kilomita 296, na litapita katika wilaya 10 (Hoima, Kakumiro, Kyankwanzi, Mubende, Gomba, Sembabule, Lwengo, Kyotera, Rakai, Kikuube), na kata 25, kabla ya kukatiza nchini Tanzania. Nchini Tanzania, litakua na urefu wa kilomita 1,147, na linapita katika mikoa 8 (Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, Tanga) na wilaya 24.

This trans-border infrastructure shall be developed and operated as a private sector project on an integrated basis by a special purpose company in which the Lake Albert Upstream Partners TOTAL, CNOOC, TULLOW, Uganda National Oil Company (UNOC), and the Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC) will be the shareholders.

Bomba hili litajengwa na kuendeshwa kama mradi wa sekta binafsi kupitia kampuni maalum (Pipe Co.) ambapo wanahisa watakuwa ni wabia wa Mkondo wa Juu wa Ziwa Albert; CNOOC LTD, TOTAL na TULLOW, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC) na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).

Kazi za Awali za ujenzi wa miundombinu ndani ya Maeneo ya Kipaumbele zinajumuisha:

- Ujenzi wa kituo cha kufunika bomba la mafuta ghafi ili liweze kutunza joto ikiwemo eneo la kuhifadhia vipande vya bomba na vifaa vya bomba ambavyo vitasafirishwa na kupelekwa kwenye kituo hicho na kuwekewa mfumo wa kuhifadhia joto;
- Kambi kuu kumi na mbili na maghala ya kuhifadhia mabomba (MCPYs) ambazo zitajumuisha makazi ya muda mfupi kwa ajili ya wafanyakazi wasio na ajira za kudumu, ofisi, jiko na bwalo la chakula na maeneo ya burudani katika kambi na maeneo haya, yatawekwa katika umbali uliokadiriwa vyema pembezoni mwa mkuza wa ujenzi. Kila kambi itakuwa na ghala la mabomba, eneo lenye mitambo ya kushughulikia maji machafu na maji taka, barabara ndani ya eneo na pengine eneo ambalo helikopta inaweza kutua na kupaa. Kambi mbili miongoni mwa kambi 12 zitatumika kama mahali pa kukusanyia kwa lengo la kusambaza mabomba katika kambi nyingine na katika mkuza linakopita bomba; na
- Ujenzi wa barabara ambazo zitakuwa zinaunganisha mitandao ya barabara zilizopo na zitakazowezesha kufikia baadhi ya miundombinu ya ujenzi na eneo la ujenzi wa bomba.

Vizuizi vya kufika katika ardhi ya Mradi wakati wa ujenzi na shughuli za uendeshaji vitaamuliwa kwa kuzingatia masuala ya afya na usalama. Eneo la Kipaumbele kwa ajili ya matumzi ya kufunika bomba la mafuta ghafi ili liweze kutunza joto, kambi kuu, eneo la kukusanyia na kutunzia mabomba yatazungushiwa uzio na kutakuwa na udhibiti wa hali ya juu hadi kufika sehemu vilipo vifaa hivi. Njia za kufika katika miundombinu iliyoko katika Maeneo ya Kipaumbele kwa Kazi za Awali zitahitajika kati ya Aprili mpaka Juni 2019. Ardhi itakayohitajika katika maeneo haya ni kama ifuatavyo:

Jedwali ES-1 – Mahitaji ya Ardhi kwa ajili ya Miundombinu ya Ujenzi

Sehemu za Mradi	Eneo Linalokadiriwa Kuathiriwa
Miundombinu ya Ujenzi – Maeneo ya Kipaumbele	
Kituo cha kufunika bomba la mafuta ghafi ili liweze kutunza joto (1 nchini Tanzania)	Hekta 40 (ekari 98.84)
Kambi Kuu 2 pamoja na Eneo la Kukusanyia vifaa	Hekta 17.6 (ekari 43.44) + hekta 18.5 (45.61) = hekta 36.1 (ekari 89.05)
Kambi Kuu za Ujenzi10/Maghala ya Mabomba (zinajumuisha maeneo 11 ambapo Kambi Kuu yenye ghala la mabomba limegawanywa katika maeneo mawili)	Kati ya hekta 17.5 (ekari 43.24) na hekta 20.9 (ekari 51.75), kwa jumla ni takribani hekta 183.5 (ekari 453)
Ujenzi na Uendeshaji	
Barabara mpya za kufikia Miundombinu ya Ujenzi , mkuza wa bomba na miundo mbinu iliyojuu ya ardhi.	Makadirio: hekta 74 (ekari 183)

Taratibu bora za utekelezaji wa viwango vya kimataifa unataka uhamishaji wa jamii uepukwe au upunguzwe pale inapowezekana kwa kutathimini michoro mbadala ya kihandisi ya mradi husika pamoja na matumizi ya vigezo mbalimbali. Njia mbadala kutoka eneo la ziwa Albert nchini Uganda kwenda maeneo tarajiwa ya upwa wa Afrika Mashariki zilitathiminiwa. Maeneo mengi ya upwa yalibainishwa na mikuza ya bomba la mafuta yenye upana wa kilometa 50 ilitathminiwa. Kupitia tafiti mbalimbali na uchambuzi, mkuza wa njia ya bomba la mafuta ghafi kwa upande wa Tanzania umechaguliwa na upana wake umepunguzwa hadi mita 30 ambapo litakuwa eneo la ujenzi na mkuza wa kudumu. Vigezo vya kitaalamu, kimazingira, kiuchumi na kijamii pamoja na urithi wa kiutamaduni vilizingatiwa jambo lililopelekea kuepukwa kwa maeneo nyeti kadhaa na kupunguza kiwango cha kuwaondoa watu katika makazi yao. Maeneo ya Kipaumbele yapo katika njia ya bomba nchini Tanzania na karibu na mtandao wa barabara uliopo Tanzania.

3. MFUMO WA KISHERIA NA KISERA

Mradi unapaswa kukidhi matakwa ya kisheria ya Tanzania kuhusu utwaaji wa ardhi, ulipaji wa fidia na uhamishaji wa watu na umedhamiriwa kukidhi viwango vya fedha vya kimataifa kama ilivyo katika Mifumo ya Udhibiti wa Mazingira Hatarishi (Kanuni za Ikweta III) na kuongozwa na vigezo vya utekelezaji vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC).

Mfumo wa Udhibiti Tanzania

Tanzania ina sheria na sera mbalimbali kuhusiana na aina ya ardhi, umilikaji wa ardhi, upataji wa ardhi, ulipaji wa fidia na uhamishaji wa watu katika makazi. Katika sheria ya Tanzania ardhi imegawanywa katika makundi yafuatayo:

- Ardhi ya Hifadhi – Ardhi iliyotengwa kwa ajili ya wanyama pori, misitu, hifadhi za majini, hifadhi za barabara na yanayofanana na hayo;

- Ardhi ya Kijiji – Inajumuisha ardhi iliyo ndani ya mipaka ya vijiji vilivyosajiliwa ambapo Mabaraza ya Maendeleo ya Vijiji na Mikutano ya Wanavijiji ina mamlaka ya kusimamia ardhi; na
- Ardhi ya Jumla – Ardhi ambayo si ya Hifadhi wala si ya Kijiji na kwa hiyo inasimamiwa na Kamishna wa Ardhi.

Ardhi kubwa itakayoathiriwa na Maeneo ya Kipaumbele ni ya Vijiji pamoja na sehemu ndogo ya maeneo ya Ardhi ya Hifadhi, sehemu kubwa inahusisha ardhi inayokatisha hifadhi za barabara zilizopo ili kuweka njia za kuingilia kwenye maeneo haya.

Wajibu wa Taasisi kwa Mazingira na Jamii

Wadau wa Utafutaji na Uzalishaji – Kampuni ya Total ya Utafutaji na Uzalishaji mafuta ya Uganda *"Total Exploration and Production (E&P) Uganda B.V. (TEPU)",* Kampuni Binafsi ya Tullow nchini Uganda "*Tullow Uganda Operations Pty Ltd*" na Kampuni ya Kitaifa ya Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Majini ya China nchini Uganda "*National Offshore Oil Corporation (CNOOC) Uganda Limited (CUL)"* – kila mdau ana sera zake zinazohusu majukumu ya kijamii na kimazingira zinazojumuisha sera za Mazingira, Afya na Usalama, mikataba ya kiitikeli, Ulinzi wa Bionuwaina mikakati ya kiutendaji katika mazingira nyeti.

Makubaliano na Serikali Iliyo Mwenyeji na Makubaliano ya Ushirikiano baina ya Serikali Mbili

Makubaliano ya Ushirikiano baina ya Serikali mbili yalisainiwa na serikali za Uganda na Tanzania tarehe 26, Mei 2017. Katika makubaliano hayo, Kipengele cha 3 kinaweka mfumo wa haki ya ardhi. Makubaliano ya Ushirikiano baina ya serikali iliyo mwenyeji na Wadau wa Mkondo wa Juu na serikali ya Uganda na Tanzania yatafuatia baada ya Makubaliano ya Ushirikiano baina ya Serikali mbili hizo. Kabla ya Makubaliano ya ushirikiano na serikali iliyo mwenyeji hayajasainiwa, Mpango Kazi huu wa Uhamishaji wa Watu na Makazi umetumia kanuni za Makubaliano ya ushirikiano baina ya Serikali mbili ambazo zinaakisiwa katika mchakato uliotumiwa kuendeleza Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa mali, njia za kutathmini na uamuzi wa fidia ya fedha au isiyo ya fedha.

Mwongozo na Viwango vya Kimataifa

Kanuni za Usimamizi wa Vihatarishi (Kanuni za Ikweta) ni nyenzo za Udhibiti wa Majanga zinazotumiwa na taasisi mbalimbali za fedha kubaini, kutathimini na kusimamia hatari za kimazingira na kijamii. Kwa kuwa mradi unaweza kuwa unatafuta fedha kutoka katika taasisi za fedha zinazozingatia mifumo ya udhibiti wa majanga, mwongozo wa mifumo ya udhibiti wa majanga kuhusu mchakato wa utwaaji ardhi, ulipaji wa fidia na uhamishaji wa watu ni muhimu na unafaa kutumika.

Viwango vya Kimataifa vya Utendaji wa Shirika la Kifedha ni seti ya viwango vinavyotoa mwongozo katika udhibiti wa majanga na athari kwa mazingira na jamii na kuongeza fursa za maendeleo. Viwango vya Kimataifa vya Utendaji wa Shirika Kifedha ambavyo vinahusika katika Mpango Kazi huu wa Uhamishaji wa Watu ni pamoja na:

- PS1: Tathmini na Udhibiti wa Majanga na Athari kwa Mazingira na Jamii;
- PS5: Utwaaji wa Ardhi na Uhamishaji wa Watu bila kupenda; na
- PS7: Makundi Maalumu.

Masuala ya Haki za Binadamu: Kama ilivyobainishwa katika mfumo wa Makubaliano baina ya serikali mbili, Mradi umekubali kuzingatia Viwango vya Haki za Binadamu katika kiwango cha kitaifa na kimataifa na kuhusu kufuata taratibu bora zinazokubalika Kimataifa, Jitihada za Misingi ya Umoja wa Mataifa ya Mwongozo katika Biashara na Haki za Binadamu.

Uchambuzi wa pengo lililopo baina ya masharti ya kisheria ya Tanzania na viwango vya Kimataifa vya Shirika Kifedha umefanyika na Mpango Kazi huu unathibitisha kuwa, pale tofauti inapojitokeza kati ya masharti ya mkopeshaji na sheria za taifa, sheria iliyo kali zaidi kati ya hizo mbili ndiyo itakayotumiwa na/au kuhusika.

4. MUHTASARI WA MPANGO, KANUNI NA MICHAKATO YA UHAMISHAJI WA WATU NA MAKAZI

Muhtasari wa Jumla wa Kanuni za Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi

Kanuni kuu za mchakato wa Utwaaji wa ardhi kwa mradi huu umewasilishwa katika Mfumo wa Sera ya Uhamishaji wa Watu. Kanuni hizi zinasisitiza haja ya mchakato wa Utwaaji wa ardhi kuendana na sheria za Tanzania na viwango vya utoaji wa fedha vya kimataifa ili kupata fedha za kuendesha Mradi.

Haki za ardhi zinazohitajiwa na Mradi nchini Tanzania kwa matumizi tofauti ya ardhi na katika hatua tofauti zinatofautisha baina ya ardhi inayohitajika kwa matumizi ya muda mfupi (wakati wa ujenzi) na ardhi inayohitajiwa kwa ajili ya muda mrefu (katika hatua ya uendeshaji). Mpango Kazi huu wa Uhamishaji wa Watu unalenga ardhi inayohitajika kwa ajili ya shughuli za muda mfupi. Ardhi hii itapangishwa kwa Mradi chini ya makubaliano ambayo bado yanajadiliwa na Serikali ya Tanzania.

Mchakato wa Upataji wa Ardhi na Uhamishaji wa Watu na Makazi

Mchakato wa jumla wa utwaaji wa ardhi kwa ajili ya Mradi umepangwa katika hatua mbalimbali zifuatazo ambazo zimewasilishwa katika Kielelezo ES-2.



Kielelezo ES-2: Mchakato wa Utwaaji wa Ardhi

Hatua ya 1 – Mfumo wa Sera ya Uhamishaji wa Watu – Mfumo wa Sera ya Uhamishaji wa Watu unahusika na upataji wa ardhi ya mradi nchini Tanzania na unaongoza hatua zote zitakazofuata katika mchakato wa upataji wa ardhi ili kuhakikisha kuwa kuna uthabiti baina ya Mpango Kazi ya kuwahamisha Watu utakaoandaliwa. Mfumo wa Sera ya kuwahamisha Watu umeandaliwa na kutolewa maoni na serikali ya Tanzania na umekamilishwa Septemba 2018 baada kupokelewa kwa maoni ya Serikali. Mfumo wa Sera ya Uhamishaji wa Watu na Makazi ulifafanuliwa kwa umma.

Hatua ya 2 – Uchunguzi na Makadirio ya Kina – yanajumuisha shughuli mbalimbali ambazo zinajazia taarifa katika Ripoti ya Uthamini kama ifuatavyo:

Kielelezo ES-2: Shughuli za Uchunguzi na Uthamini

Shughuli	Muda wa Kufanyika kwa Shughuli
Ubainishaji wa viwango vya msingi vya ulipaji wa fidia	Februari 2018
Ubainishaji wa maeneo ya ardhi kwa ajili ya upimaji	
Maandalizi ya Upimaji	
Tangazo la Upimaji na Tarehe ya ukomo	Machi 2018
Uelimishaji wa Jamii	
Upimaji wa Ardhi na mipaka	
Zoezi l la Uthamini wa mali zisizohamishika	
Uchukuaji taarifa huduma za kijamii na kiuchumi	
Uthibitisho wa taarifa za Uthamini na majedwali ya fidia	Aprili na Juni 2018
Maandalizi ya Ripoti ya Uthamini na Majedwali ya fidia	Mei - Septemba 2018
Kuweka wazi majedwali ya fidia ya fidia kwa watu waloathiriwa na mradi	Septemba – Oktoba 2018

Hatua ya 3 – Ripoti ya Uthamini wa Mali na Majedwali ya fidia – kila moja ina sehemu mbili:

- Sehemu (I): Stahiki za Tanzania; na
- Sehemu (II): Stahiki za nyongeza chini ya Matakwa ya Viwango vya Utoaji wa Fedha vya Kimataifa.

Ripoti za Uthamini zilitiwa saini na mamlaka za vijiji, kata na wilaya kama inavyotakiwa chini ya mfumo wa kisheria kabla ya kukusanywa kwa Mthamini Mkuu kwa ajili ya kuthibitishwa mwezi Oktoba 2018[1].

[1] Wakati Mpango Kazi huu wa Kuhamisha Watu na Makazi katika Maeneo ya kipaumbele ulipoandaliwa, matokeo ya mapitio ya Mthamini Mkuu na mchakato wa kuthibitisha bado yanasubiriwa. Suala lolote lililobainishwa na Mthamini Mkuu wakati wa mchakato huu litapitiwa na kushughulikiwa na Wathamini waliosajiliwa walioko katika mradi. Endapo Watu Walioguswa na Mradi watazua suala linalohusiana na uthamini katika hatua zinazofuata za Mchakato wa upataji wa ardhi masuala haya yataendelea kushughulikiwa na Wathamini Waliosajiliwa walio katika Mradi ambapo masuala hayo kama yataonekana kuwa sahihi, yatahitaji kuchukuliwa hatua za ziada za kufanya uthamini kama itahitajika.

Hatua ya 4 – Maandalizi ya Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu – Matokeo ya hatua zilizoelezwa hapo juu yameingizwa katika Mpango Kazi huu wa Kuwahamisha Watu (ambao haujumuishi taarifa kuhusu Waguswa wa mradi).

Hatua ya 5 – Uchapishaji wa Taarifa katika Gazeti la Serikali kuhusu Ubadilishaji wa Matumizi ya Ardhi na kwa Manufaa ya Umma – Ardhi itakayotumiwa katika Mradi itapatikana kwa kuzingatia kuwa inahitajika kwa manufaa ya umma. Sehemu kubwa ya ardhi iliyochukuliwa kwa ajili ya mradi itabadilishwa na Serikali ya Tanzania kuwa Ardhi ya Jumla.

Hatua ya 6 – Mikataba ya Malipo ya Fidia – Mikataba ya malipo ya fidia kwa kila Mtu aliyeguswa na mradi yataandaliwa kwa kuzingatia thamani na stahiki zilizothibitishwa katika Ripoti ya Mwisho ya Uthamini iliyoidhinishwa (Hatua ya 3) na katika Mfumo wa Stahiki (Sura ya 6 ya Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi katika Maeneo ya Kipaumbele). Makubaliano ya ulipaji wa fidia yanapendekezwa kuhusisha saini za pande tatu zifuatazo: Serikali ya Tanzania (kama 'Mtwaaji wa Ardhi') (upande wa kwanza), Mradi (upande wa pili) na Mtu Aliyeguswa na Mradi (upande wa tatu).

Maelezo kuhusu stahiki yatakuwa yakitolewa katika ngazi ya kijiji kwa kushirikiana na mamlaka za vijiji, kata na wilaya na itahusisha kuwasilisha stahiki kwa watu walioguswa na mradi (ikiwa ni pamoja na wenza wa walioguswa na mradi pale inapobidi) pamoja na kujadiliana nao kuhusu stahiki mbadala. Stahiki mbadala zitajumuisha uchaguzi kati ya fidia ya fedha au mali pale inapostahili, sambamba na uchaguzi kati ya machaguo kadhaa ya urejeshewaji wa njia za kuingiza kipato (shughuli zinazojikita kwenye ardhi, zisizojikita kwenye ardhi, n.k). Waguswa wa mradi watapewa taarifa sahihi ili kufanya uamuzi sahihi kuhusiana na ulipwaji wa fidia na mibadala ya urejeshewaji wa njia za kuingiza kipato.

Mradi huu utahusisha watu walioguswa pamoja na jamii zilizoguswa na mradi katika kufikia mwafaka wa makubaliano ya pamoja ya ulipaji fidia. Mtu anayestahili na aliyeguswa na mradi atakapokuwa amechagua aina ya fidia na aina ya urejeshewaji wa njia ya kuingiza kipato, makubaliano yatashuhudiwa na kutiwa saini na Mtu aliyeguswa na mradi. Makubaliano haya yatajumuisha maafikiano ya mwenza (pale inapobidi).

Hatua ya 7 – Ulipaji wa Fidia, Uhamishaji na Utekelezaji wa Programu za Kuwarejeshea Njia ya Kipato – Mradi huu utakua sehemu ya watia saini kwa ajili ya makubaliano ya fidia kama itakavyokuwa Serikali ya Tanzania.

Fidia ya fedha wanayostahili watu walioguswa na mradi itakuwa ikilipwa kwa awamu baada ya kutiwa saini kwa makubaliano na fedha hizo zitawekwa moja kwa moja katika akaunti ya benki ya waguswa.

Baada Waguswa kuchagua aina ya fidia na kutia saini makubaliano (Hatua ya 6), itawezekana kubainisha kwa usahihi zaidi ardhi inayohitajika kama mbadala wa makazi na mashamba. Mradi utakamilisha kupata ardhi mbadala kwa ajili ya Waguswa wa mradi waliobainishwa katika hatua ya upangaji wa Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu. Mradi utakuwa na jukumu la kuandaa viwanja mbadala kwa ajili ya nyumba mbadala kulingana na stahiki ya Mguswa wa

mradi na ramani ya nyumba iliyochaguliwa ambayo itatokana na ramani za nyumba zilizoandaliwa na msanifu majengo wa Mradi (taz. Sura ya 6).

Utekelezaji wa Kurejesha Njia ya Kuingiza Kipato na Programu za Usaidizi zitawezesha stahiki za nyongeza zinazohusiana na urejeshaji wa njia ya kuingiza kipato (taz. Sura ya 7).

Usimamizi na Tathmini unahitajika katika kipindi cha mchakato wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kuwahamisha Watu ili kuhakikisha kuwa ahadi za kuwahamisha watu na ulipaji wa fidia zinaenziwa, stahiki zinatolewa na njia za kipato zinarejeshwa walau katika hatua zinazochukuliwa kabla ya kuhamishwa (taz. Sura ya 10).

Hatua ya 8 – Utoaji wa Hakimiliki ya Ardhi kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) – Serikali ya Tanzania itahakikisha kuwa mara baada ya ardhi ya Mradi kutwaliwa na Serikali ya Tanzania, hatua zaidi zitachukuliwa ili kuhakikisha kuwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania linapewa hakimiliki ya ardhi kwa namna itakayoliwezesha Shirika hilo kuupatia Mradi mkataba wa kukodisha ardhi ambao unaofuata kanuni za Makubaliano ya Ushirikiano baina ya Serikali mbili.

Hatua ya 9 – Mkataba wa Kukodisha Ardhi Unaotolewa kwa Mradi – Mara baada ya Hakimiliki ya Ardhi ya eneo linalohitajika kwa matumizi ya Mradi kutolewa kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, Serikali ya Tanzania itapaswa kuhakikisha kuwa mamlaka zinazohusika zinaupa Mradi “Mkataba wa Kukodisha Ardhi unaofuata Masharti ya Kisheria” kwa Mradi.

Hali hatarishi – Muktadha na Vigezo

Viwango vya Utendaji vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC) nambari 5 (PS5) vinasisitiza kuwepo kwa uangalizi wa umakini wa mahitaji ya watu na vikundi vilivyo katika hali hatarishi. Mfumo wa Utoaji Stahiki (Sura ya 6) unajumuisha watu walio katika hali hatarishi kama kundi linalojitegemea. Pamoja na stahiki wanazopewa kama kaya za Watu walioguswa na mradi, wanastahili kuandaliwa programu maalumu kwa ajili ya kupata usaidizi wa kijamii.

Kwa madhumuni ya Mpango huu wa Uhamishaji wa Watu, hali hatarishi inafafanuliwa kama:

- Hali ya mtu au kikundi cha watu kukosa uwezo wa kutathmini yajayo, kumudu, kupambana na mazingira magumu;
- Watu waliokatika hali hatarishi ambao kutokana na jinsia zao, makundi ya kijamii, umri, afya ya mwili au akili, uchumi au hali ya maisha wanaweza kuathiriwa zaidi na uhamishwaji katika makazi kuliko wengine;
- Uwezo wa chini kustahimili mabadiliko na kama hawatopata msaada wa ziada wanaweza kuathiriwa kwa kiwango kikubwa zaidi na uhamishwaji wa makazi; na
- Uwezo mdogo wa kuomba au kutumia vyema msaada wa uhamishaji makazi na manufaa ya maendeleo yanayoendana nayo.

Kwa kuzingatia maandiko yaliyopo na muktadha wa maarifa ya aina mbalimbali ya maeneo ya kipaumbele, sababu mbalimbali zinazoweza kuchangia uwepo wa hali hatarishi zimebainishwa, ambazo ni:

- Jinsia ya mkuu wa kaya ya Watu walioguswa na Mradi;
- Umri wa mkuu wa kaya;
- Watu wenye ulemavu wa akili na/au viungo, na wanaoshindwa kujongea; na
- Watu walioguswa na mradi au kaya zilizoathirika zinazotegemea kilimo kama chanzo pekee katika ustawi wa maisha yao.

Sababu hizi zimetumika katika kuandaa vigezo vilivyotumika katika kubaini watu watakaoguswa na mradi. Kuna uwezekano wa kuwa na ngazi mbalimbali za hali hatarishi ndani ya kundi moja lililo katika hali hatarishi au katika maeneo tofauti ya kipaumbele kwa mfano, wanawake wote au kaya zote maskini hazifanani na hivyo hazina hali hatarishi zinazofanana. Pale itakapobainika kuwa Mtu atakayeguswa na mradi inawezekana akawa katika hali hatarishi, jitihada za ziada zitafanywa kwa mtu huyu katika hatua inayofuata ya utekelezaji ili kubaini hali zao mahususi na kuthibitisha kama wanahitaji msaada wa ziada katika mchakato wa kuhamia makazi mapya.

Mpango wa Uhamishaji wa Watu katika Maeneo ya Kipaumbele unajumuisha Mpango wa Watu Walio katika Hali Hatarishi na unapatikana katika Sura ya 8.

Makundi ya Wenyeji yaliyobainishwa kuwa Katika Hali Hatarishi katika Maeneo ya Kipaumbele

Kwa kutambua changamoto maalumu zinazoweza kuyakabili makundi yaliyo katika hali hatarishi katika kukabiliana na athari za uhamishwaji zinazotokana na utwaaji wa ardhi, sambamba na kinga inayotolewa katika viwango vya fedha vya kimataifa kwa jamii zinazoishi katika maeneo hayo, ikiwa ni pamoja na makundi maalum, hatua za ziada zinapaswa kuchulikuwa kwa makundi hayo. Mradi wa Bomba la Mafuta (EACOP) umejizatiti kuzingatia kanuni za msingi zifuatazo zinazohusu suala hili:

- Kutumia vigezo vya kimataifa na kuzingatia kuvitambua vikundi mahususi vya wenyeji walio katika hali hatarishi ambao kati yao wanaweza kujitambulisha kama makundi maalum wa maeneo hayo;
- Kuheshimu jamii ambazo zinajitambua kama wenyeji asilia kama sehemu kubwa ya ahadi ya mradi yakuheshimu haki za binadamu kwa wadau wote;
- Kupanga michakato ya ushirikishaji wa wadau na kufanya tafiti stahiki ili kuhakikisha kuwa jamii ambazo zinajitambulisha kama wenyeji asilia zinajumuishwa na kuheshimiwa katika utaratibu wa mradi unaohusisha ushirikishaji wa wadau na juhudi zinazostahili zichukuliwe. Kuweka rekodi za jitihada zote za kuheshimu jamii zilizo katika mazingira magumu na wenyeji asilia;

- Pale ambapo haki za wenyeji asilia walioathiriwa na mradi zinapokuwa zimebainishwa, kutekeleza Viwango vya Utendaji Na. 7 vya Fedha vya Shirika Kimataifa, kutambua haki za kutoa ridhaa kwa uhuru, kabla na kwa kujua na kukubaliana na jamii na kaya husika kuhusu namna ya kuzitekeleza; na
- Mradi unahusisha mchakato wa kusaidia utambuzi wa jamii zilizo katika hali hatarishi ikiwa ni pamoja na zile ambazo zinaweza kujitambulisha kama wenyeji asilia, na mradi unajizatiti katika kuchukua hatua za ziada ili kuhakikisha kuwa mahitaji yaliyoainishwa katika Viwango vya Utendaji Na. 7 vya IFC yanatekelezwa.

5. MUHTASARI WA WATU NA MALI ZILIZOATHIRIWA NA MRADI

Watu na mali ambazo zitahamishwa na/au kuathiriwa kiuchumi katika kila Eneo la Kipaumbele taarifa zao zimeandikwa kama ifuatavyo:

- Taarifa za Mkoa na Wilaya;
- Mahali lilipo eneo la kipaumbele likihusishwa na ki/vijiji cha/vya jirani na kijiji chenye mamlaka ya kisheria juu ya ardhi iliyopitiwa na Mradi;
- Data kuhusu watu na shughuli za kijamii na kiuchumi kwa ajili ya Watu walioguswa na Mradi;
- Athari za kuwahamisha kutoka eneo moja hadi lingine; na
- Kaya zilizo katika hali hatarishi.

Mpangilio wa mahali yalipo maeneo ya kipaumbele katika mikoa na wilaya katika njia ya bomba la mafuta umefafanuliwa, kuanzia Mkoa wa Kagera mpakani na Uganda na kuishia pwani katika Mkoa wa Tanga.

Jedwali lifuatalo linalotoa muhtasari wa athari za kuhamishwa kwa kila eneo linalopitiwa na mradi:

Jedwali ES-3: Muhtasari wa Athari Kuu kwa kila Eneo la Kipaumbele

	Kambi Kuu-5	Kambi Kuu -6	Kambi Kuu -7	Kambi Kuu -8	Kambi Kuu -9	Kituo na. 701	Kambi Kuu -10	Kambi Kuu -11	Kambi Kuu -12	Kambi Kuu -13	yadi ya Mabomba-13	Kambi Kuu -14	Kambi Kuu -15	Kambi Kuu -16	Jumla
Idadi ya Watu walioguswa na mradi	33	52	14	47	6	38	17	27	15	3	16	9	71	6	354

	Kambi Kuu-5	Kambi Kuu -6	Kambi Kuu -7	Kambi Kuu -8	Kambi Kuu -9	Kituo na. 701	Kambi Kuu -10	Kambi Kuu -11	Kambi Kuu -12	Kambi Kuu -13	yadi ya Mabomba-13	Kambi Kuu -14	Kambi Kuu -15	Kambi Kuu -16	Jumla
Jumla ya eneo la ardhi	25	31	10	32	10	40	15	40	27	3	10	6	70	1	320
Watu waliohamishwa	5	7	0	9	4	5	0	4	0	0	0	0	0	0	34
Idadi ya Nyumba	6	9	0	12	9	12	0	6	0	0	0	0	0	0	54
Jumla ya idadi ya watu watakaoguswa na Mradi	12	29	4	30	3	22	10	19	8	0	10	3	37	3	190
Shughuli Kuu za Kuzalisha Kipato															
Idadi ya Waguswa wa mradi wanaouza mazao ya mashamba	18	32	5	31	4	27	15	12	14	2	15	7	53	4	239
Idadi ya Waguswa na Mradi wanaofanya biashara au waliojiajiri	2	2	2	10	-	3	1	10	-	-	-	-	3	-	33
Idadi ya Waguswa wa Mradi wanaozalisha:															
Mahindi	20	29	11	37	5	33	14	24	15	2	15	-	-	4	209
Mihogo	4	33	-	10	-	3	-	2	-	-	-	-	2	3	57
Maharagwe	16	14	-	-	-	-	-	-	1	-	5	4	16	-	56
Alizeti	-	-	-	2	-	1	1	13	8	2	8	-	4	-	39
Mpunga	-	1	2	18	5	13	-	-	-	-	-	-	-	-	39
Idadi ya waathiriwa wa Mradi wanaojishughulisha na ufugaji:															
Kuku	15	23	13	30	3	32	12	15	11	2	5	-	18	4	183
Mbuzi	9	12	7	13	-	11	8	14	4	2	6	2	11	-	99
Ng'ombe	3	1	6	11	4	21	9	14	6	2	6	1	8	1	93

Takwimu zilizo katika jedwali hili ni sahihi wakati wa kipindi cha usambazaji wa Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi katika Maeneo ya Kipaumbele. Marekebisho kidogo ya takwimu yatatokea kufuatia mabadiliko ya hali ya Watu walioguswa na Mradi na maswala yatakayo ibuliwa na kikundi kidogo cha Watu walioguswa na Mradi juu ya taarifa zao za tathmini. Mabadiliko yoyote yatawekwa katika rejesta tofauti ya mabadiliko inayosimamiwa na timu inayotekeleza Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi.

6. STAHIKI, HAKI NA NJIA ZA KUTOA FIDIA

Aina mbalimbali za haki zilizofafanuliwa katika mfumo wa haki zilipangwa katika Mfumo wa Kingazi wa Uhamishaji wa Watu, kategoria maalum zilibainishwa hadi leo kutumika kwenye maeneo ya Kipaumbele kwa Mradi zimewasilishwa. Yafuatayo ni maelezo mafupi kuhusu utoaji fidia na msaada wa kupata haki kwa mujibu wa sheria nchini Tanzania na kwa mujibu wa masharti ya ukopeshaji ya kimataifa pamoja na viwango vya fidia sambamba na sheria za Tanzania zilizomo katika Sehemu I Jedwali la Fidia.

Sehemu ya I: Sheria za Tanzania

Kwa upande wa Sheria za Tanzania, msingi wa tathmini ya thamani ya ardhi na mali uliotumika unahusisha masuala yafuatayo:

- **Ardhi** – Gharama za ardhi ziliandaliwa kwa kufanya utafiti na kutumia viwango vya gharama kutoka katika ofisi ya Mthamini Mkuu. Baadaye, kulifanyika mashauriano na Mthamini aliyeteuliwa katika kila wilaya. Ili kuongeza taarifa za ziada, serikali za vijiji zilifanya utafiti ili kujua bei ya ardhi kulingana na soko. Hatimaye, viwango vya bei vilipitishwa na Mthamini Mkuu;
- **Majengo** – Uthamini wa majengo ulizingatia gharama za soko za majengo (uchakavu haukutiliwa maanani wakati wa zoezi la uthamini);
- **Mazao/Miti –** Thamani ya soko inaakisi aina ya zao/mti, kiwango cha ukuaji wake, idadi na ukomavu. Timu ya uthamini ilitumia vigezo vya mwaka 2012 kwa kila wilaya kama ilivyoagizwa na Ofisi ya Mthamini Mkuu;
- **Posho za Usumbufu –** kiasi cha asilimia 4.92 kitaongezwa katika thamani ya fidia kwa mujibu wa Sheria ya ardhi, majengo, mazao na miti ya Tanzania[2]. Kiasi hiki kinazingatia wastani wa riba inayotolewa na benki za kibiashara katika akaunti ya muda maalumu kwa mwaka na inayotumika katika jumla ya thamani ya ardhi na majengo kwa mwaka kwa mujibu wa Kanuni na. 15 ya nyongeza Na. 11 (2018) Sheria ndogo katika Sheria ya Uthamini na Wathamini Na. 7 ya mwaka 2016;
- **Posho ya Makazi** - imekokotolewa kwa kuzingatia gharama za pango kwa mwezi katika soko la Mei 2018, kwa chumba/nyumba kwa miezi 36;
- **Gharama za Usafirishaji –** ukokotozi wa gharama hii unahusisha kusafirisha tani 12 za mizigo kwa usafiri wa reli au barabara (wowote wa bei ya chini) ndani ya kilometa 20 kutoka katika eneo la makazi ya awali**;**
- **Upotevu wa Faida –** unatathminiwa kwa kuzingatia faida halisi kwa mwezi na kuzidishwa kwa miezi 36 baada ya mahesabu kuthibitishwa na mkaguzi wa fedha. Miongoni mwa watu au kaya zilizoguswa na Mradi, ni eneo moja tu ndilo linakidhi vigezo ambalo ni shamba la mkonge linaloendeshwa kibiashara ambapo kutajengwa

[2] Mthamini Mkuu wa Serikali alibainisha kuwa uwezekano wa kuwa na kiwango mbadala cha fedha za usumbufu kinaweza kuhitajika. Jambo hili kwa sasa lipo kwenye mazungumzo.

Kambi Kuu na Yadi ya Mabomba Na. 16. Hata hivyo, mmiliki wa eneo hili hajadai upotevu wa faida badala yake amewasilisha maombi ya fidia ya kuanzisha upya shughuli yake ya kumwingizia kipato; na

- **Gharama Zingine Zinazofidiwa** hasa katika maeneo ya makaburi mbinu za mkandarasi zilitumiwa kubaini gharama zinazotosha kuhamisha makaburi katika maeneo yaliyoathiriwa na Mradi.

Sehemu ya II: Haki za Ziada kwa ajili ya Viwango vya Kimataifa vya Utoaji Fedha

Sehemu ya II ya Taarifa za Uthamini na Sehemu ya II Majedwali ya Utoaji Fidia inahusisha uthamini wa haki za ziada na njia za utoaji wa fidia kwa mujibu wa mashari ya viwango vya utoaji wa fedha vya kimataifa ambavyo vinajumuisha:

- **Marekebisho ya Mfumuko wa Bei wa zao/miti kwa viwango vya mwaka 2012 –** Kwa mujibu wa Viwango vya Utendaji 5 vya Fedha kwa Shirika Kimataifa (IFC PS 5) upotevu wa mali unapaswa kufidiwa kwa kurejesha gharama za mali. Kwa hiyo, marekebisho ya mfumuko wa bei yamefanyika kwa viwango vya 2012;
- **Posho ya Usumbufu** – inatumika (sambamba na sheria za Tanzania) katika thamani ya ardhi na mali kama inavyojitokeza katika sehemu II ya Taarifa za Uthamini (kama ilivyo kwa ardhi na mali katika Sehemu ya I);
- **Ardhi Yatima** – ni sehemu ya ardhi iliyosalia baada ya ardhi yenye rutuba kuchukuliwa kwa ajili ya shughuli za Mradi. Ardhi yatima inachukuliwa kama isiyo na faida kiuchumi. Vipande vya ardhi vyenye ukubwa ulio chini ya nusu-eka vitafidiwa kwa mujibu wa Sehemu ya I katika kifungu cha 10 cha Sheria ya Utwaaji wa Ardhi ya Mwaka 1967, ambapo ardhi yatima ikizidi nusu-eka inathaminishwa kwa mujibu wa Sehemu ya II ya Ripoti ya Uthamini;
- **Ardhi na Mali katika Eneo la Hifadhi ya Barabara –** maeneo mengi ya kipaumbele yapo pembeni mwa barabara za mikoani ambapo kwa mujibu wa sheria zilizopo, hifadhi ya barabara imeongezwa. Maeneo haya ya ardhi yaliyoathiriwa hayajafanyiwa uchunguzi wala kufidiwa na mamlaka zinazohusika wakati wa zoezi la uthamini. Mradi umechunguza na kuthaminisha, na utafidia maeneo ya ardhi yaliyotumika kwa ajili ya kupanua hifadhi ya barabara;

- **Haki ya Kurejesha Uwezo wa Kuzalisha Kipato –** Kulingana na ukubwa wa athari, Mradi utatoa haki za kurejesha uweza wa kuzalisha kipato (haki inayohusiana na upatikanaji wa kipato imefafanuliwa kwa kina katika Sura ya 7);
- **Haki kwa Watu Walio katika Mazingira Magumu** – Msaada wa ziada utatolewa kwa kaya zenye mazingira magumu ambazo zinaondolewa katika maeneo yao wanayoishi na wanayofanyia shughuli zao za kiuchumi na maeneo hayo kutumiwa na Mradi; na
- **Chaguzi za Fidia** – Kwa kufuata viwango vya utendaji 5 (PS5) vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC) kaya zinazokidhi vigezo zitapewa fursa ya kuchagua ama kupewa

fidia ya pesa au fidia ya mali. Iwapo ardhi ya fidia au nyumba itachaguliwa, kiasi cha fidia ya fedha kitakatwa kutoka katika kiwango fidia ya Watu waguswa na Mradi kama inavyooneshwa katika Sehemu I ya utaratibu wa malipo ya fidia:

- **Fidia ya Ardhi** – watu wanaostahili ni pamoja na kaya ambazo zitapoteza ardhi na mazao na wameainishwa kama kundi lililo katika mazingira magumu (ikiwa ni pamoja na wale ambao shughuli zao za msingi za kujipatia kipato ni kilimo na ardhi wanayomiliki inayochukuliwa ni chini ya ekari 2 na nusu), na kaya ambazo zitapoteza kabisa makazi yake; na
- **Fidia ya Nyumba –** Kuondolewa kutoka katika eneo la makazi kutafanyika katika maeneo 6 kati ya 14 ya maeneo ya kipaumbele na mradi. Kuna jumla ya kaya 34 ambazo zitaondolewa na zimeshabainishwa zile zinazostahili kupewa fidia ya nyumba. Kaya zinazostahili zinaweza kuchagua kujengewa nyumba itakayokuwa na choo na jiko lililoezekwa au iwapo zinastahili zaidi ya nyumba moja, chaguo la ramani ya jiko na choo linatolewa vilevile.

(SEHEMU YA III NA YA IV) Fidia ya Nyumba

Kulifanyika utafiti unaohusu usanifu wa awali ili kujua aina na ujenzi wa nyumba katika maeneo ya kipaumbele na mradi kwa ajili ya kutumiwa kama msingi wa usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za fidia. Ziara katika maeneo ilihusisha kubainisha na kutoa tathmini ya aina za nyumba zilizopo, upimaji na usaili pamoja na uchanganuzi wa jumla wa makazi yaliyoathiriwa, vifaa vya ujenzi, tabia nchi na uoto. Matokeo ya uchunguzi wa uwandani, uthamini na utafiti wa mandhari ya maeneo hayo yalichukuliwa ili kuendelea kuandaa usanifu wa awali ambao unajumuisha michoro mbalimbali na ukubwa kwa kuzingatia vifaa vya ujenzi vinavyopatikana katika maeneo hayo. Michoro imeshaandaliwa kwa ajili ya majadiliano na maboresho kadiri Mradi unavyosonga mbele.

Aina kuu mbili za makazi zilizobainishwa katika maeneo ya kipaumbele na mradi ni “nyumba za jadi” na “nyumba za kisasa”. Nyumba za jadi ni zile zilizojengwa kwa kutumia vifaa vya ujenzi vinavyopatikana katika maeneo hayohayo bila kutumia saruji au mawe, na ndizo zilizo nyingi katika maeneo ya kipaumbele. Nyumba za kisasa ni zile zilizotumia vifaa vya viwandani kama vile saruji, mchanga, matofari ya kuchoma na zege.

Nyumba nyingi za makazi katika maeneo ya kipaumbele na Mradi ambapo watu na makazi yataamishwa (KAMBI KUU – 06, KAMBI KUU- 08, KAMBI KUU – 09, GHALA – Kituo cha kufunika bomba la mafuta ghafi ili liweze kutunza joto 701 na KAMBI KUU – 11) yana nyumba za jadi zilizojengwa kwa kutumia vifaa vinavyopatikana katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na nyasi na mabati, udongo (nyumba nzima), udongo na fito za miti, matofari ya udongo yasiyochomwa, matofali yaliyochomwa kwa ajili ya kuta, sakafu zilizosiribwa, zilizoezekwa kwa nyasi na kwa mabati. Baadhi ya nyumba ya jadi zinaonyesha namna wamiliki walivyokuwa wakibadili majengo yao kulingana na mahitaji na uwezo wao. Hii ni pamoja na

nyumba zilizoezekwa nyasi kuezekwa mabati na kuweka vioo madirishani. Sakafu zilizosiribwa zimefunikwa kwa nyasi ili kupungza vumbi ndani ya nyumba.

Mchanganyiko wa aina mbalimbali za makazi na yenye ukubwa uliotofautiana ulibainishwa katika maeneo ya kipaumbele ikiwa ni pamoja na mahitaji na shughuli za kitamaduni ambazo zimeathiri muundo, mahali na matumizi ya majengo madogomadogo. Nyumba za makazi zinaanzia nyumba moja hadi mkusanyiko wa nyumba zilizojengwa huku wakitumia vyoo, maliwato, majiko na stoo pamoja. Idadi ya wanakaya katika nyumba ilizingatiwa katika kuandaa mchoro wa awali. Maeneo ya Kipaumbele sita (6) tu ndiyo yenye nyumba za makazi. Kwa ujumla, kuna nyumba 54 katika maeneo ya makazi ambazo zinajumuisha nyumba 29 zenye shughuli mbalimbali na nyumba za kulala 25.

Ili kuandaa mchoro wa wazo la awali la nyumba za makazi, ulifanyika uchambuzi wa maeneo yanayotumika kama vile eneo la vyumba vya kulala, jiko, choo na maliwato (na taarifa hii imo katika Taarifa ya Mchoro wa Awali). Mtindo wa uchoraji wa ramani kwa ajili ya makazi na shughuli za kijamii katika maeneo ya kipaumbele na mradi ulizingatiwa katika kuandaa mchoro wa awali kwa ajili ya nyumba za fidia. Mchoro wa mtindo wa zamani unafaa, umeboreshwa kutokana na hali ya tabia ya nchi ya eneo husika na kwa kutumia vifaa bora vya ujenzi vilivyoandaliwa kwa kuzingatia uchumi.

Mkakati wa kutumia mchoro unaotumika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za fidia katika maeneo ya kipaumbele umezingatia taratibu bora za ujenzi na viwango vinavyotambulika na vipimo vya kitaalamu kama vilivyotolewa na taasisi zilizoidhinishwa na kujumuisha yafuatayo:

- Mfanano wa eneo la sakafu/ukubwa wa eneo la kujenga nyumba, yaani kutumia mbinu ya kujenga makazi kwa kuzingatia ukubwa wa makazi ya awali;
- Uimara na urahisi wa ujenzi;
- Kiwango cha chini cha ukubwa wa nyumba kinachoweza kutimiza mahitaji ya starehe, kiafya, kiusalama na kitamaduni ya Watu walioguswa na Mradi. Aidha, sababu za eneo dogo la sakafu na uwezo wa kumudu miundo hiyo (rejea viwango na vipimo vya TBS - ISO/TC 59/SC15 katika ‘Mfumo wa Ufafanuzi wa Kufaa kwa Nyumba za Makazi’);
- Kwa kila nyumba ya fidia kuwe na eneo la shimo moja la choo linalotoa hewa linalokidhi viwango na jiko lililoezekwa (lililo wazi, sio lililozungushiwa ukuta); na
- Mguswa wa Mradi ambaye anastahili kufidiwa zaidi ya nyumba moja (1) atapewa uchaguzi wakuchagua watachagua ama:
  - Choo cha kisasa kilichoboreshwa na jiko lililoezekwa kwa kila nyumba ya fidia; AU
  - Bafu na Choo kimoja vya kisasa, jiko lililoezekwa pamoja na stoo kwa kila nyumba kadhaa pamoja.

Viwango vya ukubwa wa nyumba vimeshaandaliwa kwa ajili ya maeneo ya kipaumbele na mradi na vimewasilishwa katika Sura ya 6 ya Mpango wa Makazi ya Fidia.

(SEHEMU YA V): ARDHI YA FIDIA

Watu walioguswa na Mradi wanaostahili fidia ya ardhi watapewa nafasi ya kuchagua kati ya kupewa fidia ya ardhi au fedha (au mchanganyiko wa vyote viwili). Kanuni hiyo itatumika pia kwa wale watakaoondolewa katika makazi. Watu walioguswa na Mradi wanaostahili watapewa fursa ya kuchagua kati ya fidia ya fedha na kupewa ardhi/nyumba wakati wa vikao vya kuelezwa haki zao, ambavyo vitakuwa moja ya hatua za mwanzo katika utekelezaji wa Mpango wa Kuwaondoa Watu na Makazi. Kwa hiyo, mahitaji ya fidia ya ardhi yaliyoingizwa katika waraka huu yametokana na mawazo kwamba watu wote walioguswa na mradi wanaostahili fidia ya ardhi na/au makazi watachagua makazi badala ya kuchagua fedha (au mchanganyiko).

Upotevu wa makazi utatokea katika Maeneo sita ya Kipaumbele: KAMBI KUU -05, KAMBI KUU -06, KAMBI KUU -08, KAMBI KUU -09, KITUO NAMBA 701 na KAMBI KUU-11. Viwanja vya makazi vitahitajika kwa ajili ya kujenga nyumba kwa wale watakaondolewa katika makazi.

Wakati wa uchunguzi wa maeneo ya fidia ya ardhi, maeneo 60 yalibainishwa kuwa yangeweza kuwa yanafaa kwa ardhi ya kilimo, maeneo ya nyumba za kuishi au mchanganyiko wa haya mawili. Jumla ya maeneo 45 yalitembelewa na timu za wakaguzi wa maeneo kukiwa na baadhi ya maeneo yaliyokataliwa kuwa hayafai, ama kabla au baada ya kutembelea maeneo husika.

Wakati huohuo ufuatiliaji wa kukamilisha utafiti zaidi wa Mpango Kazi wa Kuhamisha watu na makazi Mradi umekuwa na unaendelea kutekeleza tafiti zaidi kwa kushirikiana na wahusika waliopangwa katika kutambua ardhi ya fidia na nyumba ya kuishi kwa muda mfupi, pamoja na tafiti zaidi zinazofanyika katika maeneo yote ili kutwaa ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Kuwaondoa Watu. Zoezi hili limebaini ardhi ya ziada kwa ajili ya utekelezaji wa mradi pamoja na chaguo la kupata nyumba nyingine za kuishi kwa muda mfupi karibu na maeneo kadhaa ya kipaumbele. Matokeo ya taarifa hizi yatawasilishwa katika jumuiya na watu walioguswa na mradi pamoja na watu walioguswa na mradi wakati wa vikao vya kuwafahamisha haki zao katika maeneo yao binafsi. Utoaji wa taaarifa kuhusu suala hili utafanyika ili kuondoa uwezekano wa kuwepo fununu.

7. Mpango wa Kurejesha Uwezo wa Kuzalisha Kipato

Mkabala wa Mradi wa kurejesha uwezo wa kuingiza kipato umewasilishwa katika Mpango wa Kuwarejeshea Watu Uwezo (LRP) iliyo katika Mpango kazi wa Kuhamisha watu na Makazi. Programu zilizo katika mpango wa kurejesha uwezo wa kuingiza kipato zimebuniwa kurejesha na inapowezekana kuboresha ustawi wa watu baada ya kuguswa na mradi katika makazi yao na kiuchumi. Ili kustahili kuingia katika programu hizi inategemea na ukubwa wa athari kwa Watu walioguswa na mradi. Program za mbinu za kumudu maisha na zingine inategemea na ustahili wa Mguswa kama amechagua kupata fidia ya ardhi au ya fedha taslimu.

Viwango vya utendaji bora kimataifa vinasisitiza umuhimu wa kuboresha vipato vya kaya zilizoathiriwa kwa kuhamishwa (kwa kuondolewa katika makazi na kuodolewa katika njia za uchumi) kwa kuweka mkakati kabambe wa kuboresha njia za kuzalisha kipato cha wahusika. Kimsingi, Taasisi za Fedha za Kimataifa zinaeleza kuwa hatua za uboreshaji wa njia za kuzalisha kipato zinapaswa kuwa sahihi kiutamaduni na endelevu; yaani, zinapaswa kuzingatia uwezo wa ndani na zinapaswa kuwezesha Watu walioguswa au kaya kujitegemea badala ya kutegemea rasilimali za nje (kama vile mtaji uliotolewa na mradi na utaalamu) katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Uhamishaji wa Watu.

Mpango wa Kurejesha Njia za Kuzalisha Kipato unatoa mwelekeo wa hali ya maisha na kijamii na kiuchumi inayopatikana kwenye maeneo mbalimbali ya Kipaumbele, na unaelezea kiwango cha shughuli za kurejesha njia za kuzalisha kipato zinazotarajiwa na programu za mahali husika pamoja na mifumo ya kusaidia inayoweza kutumika katika utekelezaji Mpango wa Kurejesha Uwezo wa Kuzalisha Kipato kwa Maeneo yanayolengwa na Mradi. Shughuli zinazopendekezwa za kurejesha njia za kuzalisha kipato na mapendekezo ya chaguzi kwa Watu walioguswa na mradi zimewasilishwa. Huu waraka wa Mpango wa kuhamisha watu, utakuwa ni waraka hai na unaweza kurekebishwa kutokana na mabadiliko yanatakayotokea kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Uhamishaji wa Watu.

Lengo kuu la Mpango wa Uhamishaji wa Watu na Makazi na lililosisitizwa katika mbinu ya kuandaa Mpango wa Kuhamisha Watu, ni kuhakikisha kunakuwa na maboresho yanayoonekana katika maisha na njia za kuzalisha vipato vya waathiriwa wote. Malengo mahususi ya Mpango wa Uhamishaji wa Watu ni:

- Kutoa machaguo ya njia za kuzalisha vipato vilivyo endelevu kwa kaya zilizoathiriwa na mradi;
- Kuweka mfumo wa kutumia fursa kikamilifu kwa wale wanaopokea fidia ya fedha;
- Kuwezesha kujitegemea (yaani, kuepuka hatari ya kuwa tegemezi katika kupata chakula) na kuendeleza uwezeshaji wa kijamii na kiuchumi.

Kaya nyingi katika Maeneo ya Kipaumbele zinategemea ardhi yao kwa ajili ya kujikimu na mapato ya fedha. Kaya zinazotegemea chanzo kimoja cha mapato kwa ajili ya kuishi zipo katika hatari zaidi ya kupata mitikisiko inayosababishwa na matukio kama vile mchakato wa uhamishaji wa watu na makazi. Kaya za Watu walioguswa na mradi ambazo kipato chao kinatokana na shughuli za kuingiza kipato ambazo zitaathiriwa zaidi na Utwaaji wa maeneo ya Kipaumbele na ambazo hazina njia nyingine yoyote ya kutegemea, zitakuwa katika hatari zaidi ya kupata mtikisiko. Kwa wastani, utafiti wa kijamii na kiuchumi kwa maeneo ya kipaumbele ulionyesha kwamba familia inahitaji angalau ekari 2.5 za ardhi kwa ajili ya mahitaji ya chakula na mahitaji ya fedha[3].

[3] Kaya ambayo inalima shamba la ekari zaidi ya moja ilikuwa na alama ya ya 2.4 zaidi ya wastani ukilinganisha na wale ambao wanalima shamba la chini ya ekari moja (2.5 ekari) – VAM, 2010. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 2009/10 Tathimini ya Utoshelevu wa Chakula na Uchambuzi wa Kiusalama.

Athari za njia za kuzalisha kipato zimetathminiwa kuzingatia Mpango wa Maisha Endelevu wa DFID. Hii inahakikisha kwamba tathmini ya jumla inafanyika kwa kuzingatia athari za asili, kieneo na kifedha pamoja na kiwango cha madhara katika masuala ya kijamii na ya kibinadamu katika mikakati ya kuzalisha kipato.

Mradi utatoa msaada wa kurejesha njia za kuingiza kipato kutegemea ukubwa wa athari katika mkakati wa kuhamisha Waguswa wa mradi, uwezo wao wa kustahimili na uwezo wao wa kurejesha njia za kuzalisha kipato. Kutokana na kupitia athari katika njia za kuzalisha vipato, vigezo viliwekwa ili kutambua aina ya msaada wa kuzalisha kipato utakaotolewa kwa makundi ya Watu walioguswa. Mpango huu umeandaliwa kwa kuzingatia vigezo vya njia za kuzalisha kipato katika ngazi ya kikundi, na baadhi ya Waguswa wakihitaji kupata msaada kwa kiwango fulani katika ngazi binafsi wa kurejesha njia za kuzalisha kipato kutokana na ukubwa wa athari kwao (kwa mfano kuondolewa katika makazi). Inachukuliwa kuwa Waguswa mradiwaliohamishwa makazi na wale walio katika hali hatarishi wanaweza kuhitaji msaada katika ngazi binafsi kwa kiwango fulani ili kurejesha njia za kuzalisha kipato na/au kuhitaji kupata msaada wa kuingia katika programu za kuzalisha kipato katika ngazi ya kikundi.

Jedwali ES 4: Vigezo vya Kustahili Kurejeshewa Njia za Kuzalisha Kipato

Kundi	Vigezo	Aina ya Msaada wa Kurejesha Njia za Kuzalisha Kipato
Kundi 1	Watu maalumu walioguswa na Mradi watapoteza kabisa makazi au kukutana na vigezo vya hali hatarishi na kupoteza ardhi[4]	Programu za kurejesha njia za kuzalisha kipato katika ngazi binafsi na programu za kutegemea ardhi na zisizotegemea ardhi za kurejesha njia za kuzalisha kipato katika ngazi ya kikundi
Kundi 2	Watu maalumu walioguswa na Mradi watapoteza ardhi na mazao au miti, lakini hawatapoteza makazi.	Programu za kutegemea ardhi na zisizotegemea ardhi za kurejesha njia za kuzalisha kipato katika ngazi ya kikundi.
Kundi 3	Watu maalumu walioguswa na Mradi watapoteza mazao, miti au mali nyingine, lakini sio ardhi au makazi, na jumla ya thamani ya fedha ya fidia ni TSh 100,000/= au zaidi.	Kurejesha njia za kuzalisha kipato kwa vikundi bila kutegemea ardhi (yaani mafunzo ya usimamizi wa fedha na ujasiriamali).
Kundi 4	Watu maalumu walioguswa na Mradi watakuwa na fidia ya jumla ya <TSh 100,000/=	Hakuna fidia ya njia za kuingiza kipato itakayotolewa ni fedha tu.

Katika majadiliano na wadau, mada kuu iliyotolewa ni haja ya kuimarisha shughuli za kilimo ili kuzuia upungufu wa chakula na fedha, hasa wakati wa ukame. Jambo lingine lililohusiana na hili ni upatikanaji wa mavuno, vifaa vya kuhifadhi mazao yasiharibiwe na wadudu na upatikanaji wa maji kwa mwaka mzima. Shughuli zisizo za kilimo hazikuwa ajenda muhimu; hata hivyo, ilitolewa hoja kuhusu fani ya usanii na kuendeleza stadi za ujasiriamali kwa vijana.

Njia za kurejesha uzalishaji wa kipato zinazopatikana kwa Watu walioguswa na Mradi zimeorodheshwa hapo chini na shughuli za kurejesha uzalishaji kipato zinazoandaliwa katika maeneo husika zimewasilishwa. Programu hizi zinaweza kubadilishwa na zitaendelezwa zaidi wakati wa utekelezaji.

[4] Sehemu ya 4.3 – Watu walioguswa na mradi watatambuliwa kama waguswa. Mbinu za kuwasaidia watu hawa walioguswa zitaandaliwa kwa kina zaidi kuhakikisha kuwa wanapata programu za makazi mapya na zimeandaliwa kulingana na mahitaji.

Jedwali ES-5: Kurejesha Njia za Uzalishaji kipato

Njia za Kurejesha Uzalishaji Kipato - Vikundi 1 na 2 (Kundi 1 Watu walioguswa na mradi watapewa fursa ya misaada binafsi na wa ziada uliolenga kupata programu hizi za kusaidia kurejesha uzalishaji kipato	
(Vikundi 1 na 2) Vikuu– Kaya zote zinazostahili:	**Fidia ya Ardhi** *(kwa wale wanaostahili)* – kulingana na gharama ya ardhi iliyopotea[5].
	Maandalizi ya Ardhi na Upandaji katika Ardhi ya Kilimo-Iliyofidiwa Maeneo yote yanayopewa Kipaumbele. (Isipokuwa KAMBI KUU- 16)
	Programu ya Kuboresha Mahindi (Urejeshaji wa Njia za Kuingiza Kipato 2) (Maeneo yote isipokuwa KAMBI -14 na KAMBI 15 kwa kuwa mahindi hayalimwi katika maeneo haya)
	Bajeti za kaya na Mafunzo ya Usimamizi wa fedha (Urejeshaji wa Njia za Kuingiza Kipato 8)
	Maendeleo ya Biashara (Urejeshaji wa Njia za Kuingiza Kipato 7)[6] (Kila kaya inayostahili kupata aina moja ya usaidizi)
Chaguo (Kikundi cha 1 na 2) - kila kaya inastahili kupata chaguo moja, isipokuwa: KAMBI KUU 14 na KAMBI KUU 15 kwa watu walioathiriwa na Mradi ambao watastahili kuwa na chaguzi mbili:	Aina ya 1: Programu ya Ufugaji Kuku (Urejeshaji wa Njia za Kuingiza Kipato 4)[7]
	Aina ya 2: Programu ya Ufugaji Bora (Urejeshaji wa njia za Kuingiza kipato 5)
	Aina ya 3: Mazao Mchanganyiko (Urejeshaji wa njia za kuingiza kipato 3)
	Aina ya 4: Ufugaji Bora wa Nyuki (Urejeshaji wa njia za kuingiza kipato 6)[8]
Machaguo ya Kurejesha Njia za Kuzalisha Kipato – Kundi 3 (yaani wapangaji wa kilimo)	

[5] Endapo hakutakuwa na maeneo ya kutosha ya kuwafidia Walioguswa katika maeneo ya kipaumble, wamiliki wa sasa wa ardhi au Walioguswa wataomba fidia ya fedha na ardhi. Mpaka ukubwa wa ekari 3.5 kwa kaya utatolewa. Kaya zitafidiwa eneo lingine lolote litakalokuwa limechukuliwa kutokana na Mradi. Usaidizi utatolewa kwa kaya zitakazoathirika kupata maeneo ya kilimo kama itahitajika.

[6] Katika makazi mapya mafunzo ya shughuli mbalimbali ya kujenga uwezo yatatolewa. Mradi utafikiria pia kuwasaidia Waguswa kupata nafasi za mafunzo ya ufundi stadi.

[7] Hakukuwa na ufugaji wa kuku wakati wa ukaguzi wa KAMBI -14, Mradi utaangalia iwapo shughuli mbadala inaweza kutolewa katika maeneo ya kipaumbele na endapo Walioguswa na mradi watapenda shughuli hizo.

[8] Ufugaji wa nyuki ulibainishwa katika maeneo ya kipaumbele –KAMBI -06, KAMBI-08, STOO 13, GHALA – Kituo cha kufunika bomba la mafuta ghafi ili liweze kuhifadhi joto 701 KAMBI-10, KAMBI-11, KAMBI-12 na KAMBI-16 – katika mikoa saba ambapo maeneo ya kipaumbele yanapatikana.

(Kundi 3) Kuu – Kaya zote zinazostahili zinapata:	**Kuendeleza Biashara** (Urejeshaji wa njia za kuingiza kipato 7) (Kaya zote zinazostahili zinapata aina moja ya usaidizi)
	Mafunzo ya Upangaji wa bajeti ya Kaya na Matumizi ya Fedha (Urejeshaji wa njia za kuingiza kipato 8) (Katika Maeneo yote)
Chaguzi (Kundi 3) – Kila kaya inastahili kupata aina moja ya chaguzi:	Uchaguzi A: Programu ya Uzalishaji wa Kuku (Urejeshaji wa njia za kuingiza kipato 4)
	Chaguo B: Ufugaji Bora wa Nyuki (Urejeshaji wa njia za kuingiza kipato 6)

Msaada Katika Kipindi cha Mpito

Msaada katika kupindi cha mpito utatolewa kujazia malipo ya fidia ili kuhakikisha kwamba kaya zinaweza kukidhi mahitaji yao ya msingi na kudumisha hali yao ya maisha baada ya kupoteza ardhi yao hadi wanapokuwa na fursa ya kurejesha njia zao za kuzalisha kipato kabla ya mradi kuanza. Huduma hizi za awali ni pamoja na:

- Msaada wa kipindi cha mpito ni pamoja na kupatiwa vikapu vya vyakula na vitu vingine kuhakikisha kuwa kaya zinapata chakula wakati wa kipindi cha mpito; na
- Mafunzo ya usimamizi wa fedha kwa kaya zote zinazopokea fidia ya fedha ili kuzipatia kaya stadi na ujuzi wa kusimamia fedha walizopata.

Msaada wakati wa kipindi cha mpito utahusisha hasa "kikapu cha bidhaa". Kikapu chenye bidhaa kinazingatia tafsiri ya Umoja wa Mataifa ya Kikapu cha Chakula ambacho kinatoa: nafaka, mchele, kunde, mafuta, na chumvi. Vitu vinavyotolewa kwa kila kaya (ikikadiriwa kuwa na wastani wa wanakaya 6) kwa mwezi, itatumika ili kutoa chakula kitakachotumiwa na waathiriwa katika maeneo ya vipaumbele tofauti kwa kushauriana na Afisa wa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya na Watendaji wa Kata. Kaya zilizoathiriwa zaidi na zilizo katika hali hatarishi zitafuatiliwa kwa karibu ili kujua kama msaada uliotolewa unatosha na kuamua kama kuna marekebisho yoyote yatakayohitajika katika kikapu cha bidhaa.

Kwa wale wanaostahili kupata msaada wakati wa kipindi cha mpito, wanaweza pia kustahili msaada maalum wa matibabu wakati wapo kwenye hii programu. Gharama zitalipwa moja kwa moja kwa mamlaka husika, baada ya kutoa uthibitisho kama vile bili. Gharama nyingine zinazohusiana na kubadili shule (vitabu, sare za shule, na kadhalika) zitagharamiwa pia na programu. Programu ya Mfuko wa Maendelo ya Jamii (TASAF) hutenga kiasi cha shilingi za Kitanzania 2,000/- kwa kila mtoto anayekwenda shule kwa mwezi. Mwanafunzi atatakiwa kuwa na mahudhurio ya 75% shuleni ili aweze kuendelea kupata ufadhili huo.

8. MPANGO WA WATU WALIO KATIKA HALI HATARISHI

Mpango wa watu walio katika hali hatarishi umefafanuliwa katika Mpango wa Kuwahamisha Watu na Makazi na umeonyesha namna Mradi umedhamiria kuthibitisha hali ya Waguswa wanaoweza kuwa katika hali hatarishi, kama ilivyobainika katika mchakato wa utafiti na kufanyia kazi athari zilizobainika. Hii inahusisha kuhakikisha kuwa Waguswa hao wanajulishwa kuhusu shughuli za mradi na wanasaidiwa kukabiliana na athari nyingine zitakazotokana na shughuli za mradi.

Malengo ya Mpango wa Watu walio katika hali hatarishi ni:

1. Kuhakikisha kuwa watu na kaya zilizo na zinazoweza kuwa katika hali hatarishi zinaainishwa na kufuatiliwa kabla na baada ya mchakato wa kuhamishwa, ili kuweza kufuatilia hali zao za maisha na kujua mafanikio ya fidia, kusaidia urejeshaji wa njia za kuingiza kipato;
2. Kutoa msaada unaotakiwa kwa kaya zilizobainishwa kuwa kwenye hali hatarishi katika kuanzisha maisha mapya (ikiwa ni pamoja na wale waliohamishwa makazi). Wanafamilia wa kaya zilizo katika hali hatarishi wanaweza kuhitaji msaada maalum katika kuanzisha makazi mapya kwa sababu wana uwezo mdogo wa kumudu athari za kuhama tofauti na wanakaya wa kawaida;
3. Kubainisha fidia na huduma za kuwarejesha katika hali ya awali watu walio katika hali hatarishi ambazo zinajumuisha misaada ya ziada, na kutumia zaidi njia za kuondoa hali hatarishi zilizo na athari kidogo zaidi pale inapowezekana;
4. Kuwasaidia watu waliobainishwa kuwa wako kwenye hali hatarishi ili waelewe kikamilifu machaguo yao ya kuhama na kupata fidia, na kuwahimiza kuchagua chaguo lenye athari kidogo zaidi;
5. Kuzingatia kwa makini mitandao ya kijamii inayohusu miundo ya kifamilia na kikabila na kuona namna ambavyo mitandao hii inaweza kuanzishwa tena katika makazi mapya hususan kwa watu walio katika hali hatarishi kwa mfano kuhakikisha miundo ya msaada katika maeneo ya kuhamia yanazingatiwa; na
6. Kubainisha hatua nyingine za ziada kwa ajili ya makundi yaliyo katika hali hatarishi ili kuweza kustahimili athari zinazotokana na Mradi wakati wa kuhamia katika makazi mapya, hasa kuwa makini na wanawake wajawazito, watoto, wazee, na watu wenye ulemavu.

Katika muktadha wa kuhamishwa na utwaaji wa ardhi dhana ya ‘makundi yaliyo katika hali hatarishi’ anapewa mtu binafsi, kaya, au kikundi cha watu ambao wanaweza kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na mchakato wa kuhamisha watu kwa kuzingatia jinsia, kabila, umri, ulemavu wa viungo au akili, hali ya kiuchumi au hali ya kijamii katika jamii yao. Ni muhimu kutambua kwamba viwango tofauti vya hali hatarishi vinaweza kuwa ndani ya kikundi au kuathiri katika maeneo mbalimbali ya vipaumbele kutokana na hali za wahusika kuwa tofauti, maathalani wanawake wote au kaya zote maskini hazifanani na kwa hiyo hali ya mazingira yao kiusalama haifanani. Seti kamili ya huduma zitakazo tolewa kwa kila aliyethibitika kuwa katika hali hatarishi na kaya zitatathminiwa tofauti tofauti, hivyo usaidizi utatofautiana kulingana na mahitaji yao maalum yatakayobainika.

Inaweza kuthibitishwa wakati wa kuendelea kufanya kazi na Watu walioguswa na mradi kuwa sababu hizi za hali hatarishi zinaweza zisiathiri uwezo wao wa kuanzisha njia za uzalishaji kipato na athari kuanzia Utwaaji wa ardhi sio lazima ziwe na uhalisia kwao. Mradi huu umetumia mbinu ambayo wale walio katika maeneo ya kipaumbele, wanachukulia sababu hizi kama seti ya 'vigezo vya uchunguzi' ili kutambua hali hatarishi ambayo inataka juhudi za ziada zitumike kwa Watu walioguswa na mradi. Hizi juhudi za ziada zinahitajika ili kuthibitisha kama mambo haya yanaweza kuathiri uwezo wao wa kurejesha shughuli za kuingiza kipato na kama athari zinazohusiana na Mradi hazitakuwa na uhalisia kwa Watu walioguswa na mradi.

Mpango wa watu walio katika hali hatarishi unazingatia kipengele maalum cha hali hatarishi kuhusiana na makundi kadhaa, ambayo ni:

- Wanawake na Watoto;
- Wazee;
- Watu wenye ulemavu; na
- Vikundi vya walio katika hali hatarishi na/au Jamii.

Kipengele muhimu cha kusaidia makundi yaliyo katika hali hatarishi ni kuhakikisha kuwa wanapata nafasi ya kushirikishwa katika kufanya maamuzi ili waweze: a) kupata taarifa za kutosha kuhusu mradi, ikiwa ni pamoja na athari na fursa zinazowafaa; na b) wanaweza kujibu na kutoa maoni katika mchakato wa kuandaa shughuli wanazoshirikishwa.

- Vikundi vingine vilivyo katika hali hatarishi vimebainishwa kutokana na ugumu unaoweza kutokana na kuchukuliwa kwa ardhi na mabadiliko ya shughuli za kuzalisha kipato na/au wanachama wa vikundi vya kijamii ambavyo vinaweza kujitambulisha kama makundi maalum kwenye jamii (yaani KAMBI KUU-12, KAMBI-13 na STOO-13). Mashauriano na haya makundi ni sehemu muhimu ya mbinu kuu ya mradi kuwashirikisha wanajamii kwa jumla kwa lengo la kujenga uaminifu na ushirikiano wa wanajamii katika Mradi huu, kwa kuhakikisha kuwa ushirikishwaji na ushiriki unaozingatia uelewa wa mlengwa unafanyika na kupitia uelewa na ufuatiliaji wa namna ambavyo athari zinadhibitiwa na matumizi ya viwango vya kimataifa.

Mbinu hii kabambe iliyopangwa katika Mfumo Shirikishi wa Wadau wa Mradi, Mpango Shirikishi wa Wadau, Miongozo ya Ushirikishaji wa Wadau na Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko ya Wanajamii ni muhimu kwa wadau na jamii zilizoathiriwa ikiwa ni pamoja na vikundi vilivyo katika mazingira magumu au watu binafsi. Utaratibu huu unaruhusu makundi maalum kwenye jamii au watu binafsi kutoka katika makundi maalum walio na haki ya kupata ushauri wa ziada ikiwa ni pamoja na utoaji idhini unaofanyika kwa uhuru, uelewa na ufahamu kabla ya mradi kuanza kuhakikisha kuwa mahitaji yao ya ushauri yanatekelezwa bila kuleta mvutano wowote kwa matarajio ya ushirikishwaji na ushiriki unaozingatia uelewa wa mlengwa kwa wadau wote wa mradi.

Posho inatolewa kwa ajili ya mashauriano tofauti ya siri na vikundi, kaya au watu binafsi kama hili linaonekana kuwa muhimu ili kuhakikisha kuwa makundi haya muhimu yanasikilizwa (k.m. wanawake walioathiriwa na mradi, watu wenye ulemavu walioguswa na mradi)

Watu na kaya tofauti zitahitaji misaada ya viwango tofauti na usaidizi wakati wa utekelezaji wa uhamishaji wa watu, kulingana na hali hatarishi husika.

Juhudi za kipekee za kulinda na kusaidia makundi yaliyo katika hali hatarishi ambazo zinaweza kufanywa zinajumuisha:

- Kuhakikisha makubaliano ya ulipaji wa fidia yanakuwa na ridhaa ya mwenza;
- Kubainisha njia za kusaidia kupunguza majukumu ya wanawake na kuboresha huduma za kifamilia;
- Kuongeza uthabiti wa kifedha kupitia programu ya usimamizi wa fedha, kwa mfano kwa kuvisaidia vikundi vya kukopeshana, kutoa mafunzo ya stadi mbalimbali, kusaidia kupata masoko;
- Kusaidia maendeleo ya elimu hususani kusoma, kuhesabu na kuandika;
- Kuimarisha ushiriki wa makundi yaliyo katika hali hatarishi katika michakato ya kutoa maamuzi;
- Kuweka fursa sawa za ajira katika Mradi;
- Kutoa kipaumbele kwa mahitaji ya watu na makundi yaliyo katika hali hatarishi wakati wa kuchagua maeneo ya kufidia nyumba/kufidia ardhi pale inapowezekana;
- Kutoa msaada kwa makundi na watu walio katika hali hatarishi wakati wa kubomoa na kuhamisha mali zao;
- Kutoa msaada (si pesa za fidia pekee) kwa makundi yaliyo katika hali hatarishi pale ambapo ujenzi wa jengo utahitajika tena na;
- Kuhakikisha watu walio katika hali hatarishi wanapewa kipaumbele katika programu za kuwarejeshea njia za kuingiza kipato.

Mpango wa Watu walio katika hali hatarishi unaenda sambamba na utekelezaji mpana wa Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na utakamilika pale ambapo njia ya uingizaji kipato ya watu walio katika hali hatarishi itakapokuwa imerejeshwa walau katika kiwango kilichokuwapo kabla ya Mradi. Mpango wa Watu Walio katika hali hatarishi unaweza kuboreshwa wakati wa programu ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu.

Shughuli zote za kusaidia makundi yaliyo katika hali hatarishi zimeorodheshwa na kunakiliwa katika Rejesta ya Makundi na Kaya Zilizo katika hali hatarishi, shughuli za ufutiliaji zinaweza kujumuisha:

- Ushirikishaji unaoendelea wa Kamati ya Maendeleo ya Kijiji (inapokuwepo) kama sehemu ya kufuatilia kaya zilizo katika hali hatarishi;
- Kubainisha na kuweka kumbukumbu ya taarifa za watu na kaya zilizo katika hali hatarishi kwenye Rejesta ya Makundi na Kaya Zilizo Katika hali hatarishi;
- Kufuatilia hatua zote zilizoanzishwa kuwasaidia watu na kaya zilizo katika mazingira magumu kupitia mchakato wa ulipaji wa fidia na shughuli za urejeshaji wa njia za kuingiza kipato; na
- Kufuatilia urejeshaji wa njia za kuingiza kipato.

Timu za ushirikishaji wa wadau zitakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa mbinu za ziada za ushirikishaji zinatumika ili kuwezesha ushiriki wa makundi yaliyo katika hali hatarishi. Timu ya uwekezaji katika jamii ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki itakuwa na jukumu la kusimamia ushiriki wa watu walio katika hali hatarishi kwenye miradi sahihi ya kijamii. Jukumu la kuratibu na kufuatilia hali za watu walio katika mazingira magumu na shughuli husika za msaada zinaangukia ndani ya mawanda ya Timu ya Utekelezaji wa Urejeshaji wa Shughuli za Kuingiza Kipato, jukumu hilo litakuwa likipitiwa mara mbili kwa mwaka.

9. MASHAURIANO NA UWAZI

Mradi wa EACOP umedhamiria kuhakikisha wadau wake wote wanashiriki kikamilifu kulingana na kanuni za ushiriki, kuheshimu haki za binadamu, kutokua na ubaguzi, kujenga uwezo, uwazi na uwajibikaji. Hivyo ushirikishwaji wa wadau utafanyika ili: kuelewa na kuheshimu wadau wote; Kuanzisha uhusiano chanya na wa kudumu na wadau; Kutoa taarifa za mradi ili kuwawezesha wadau kushiriki kikamilifu katika mchakato wote; Kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau ili kuelewa matatizo yao na kuyatafutia ufumbuzi; Kushughulikia matatizo ya wadau kwa kuzingatia haki na ufanisi; na kutaarifu wadau juu ya Mfumo wa Jamii wa Kuwasilisha Malalamiko ili waweze kuutumia pale inapohitajika na kuwasilisha malalamiko waliyonayo juu ya mradi.

Mashauriano na wadau ni sehemu muhimu ya mpango wa kuwahamisha watu, uwazi na michakato ya utekelezaji. Mashauriano ni muhimu ili kuhakikisha kuwa katika hatua jamii zilizoathiriwa zinapata fursa, pamoja na wadau wanaovutiwa kuweza kutoa maoni yao katika Mchakato wa Mpango wa Uhamishaji wa Watu na kusaidia kuelekeza kipaumbele, mchakato na matokeo.

Malengo ya Mradi ya ushirikishaji wenye tija wa wadau ni:

- Kuhakikisha kuwa wadau wa ndani wanapata taarifa mapema kuhusu shughuli za Mradi;

- Kujenga imani na kuungwa mkono na jamii pana kwa ajili ya ushughuli za baadaye kupitia uelewa na ufuatiliaji wa namna athari zinavyosimamiwa na namna viwango vya kimataifa vinavyozingatiwa;
- Kuhakikisha kuwa ushirikishaji unafanyika kwa namna inayoratibiwa vizuri kwa kutumia kanuni zilezile, viwango vilevile, taarifa, n.k.;
- Kupata utaalamu wa asasi za kiraia, stadi au rasilimali za kuzisaidia, kwa mfano uwekezaji katika jamii, uanzishaji na utekelezaji wa mradi wa urejeshaji wa shughuli za kuingiza kipato, kuweza kutumia bidhaa na huduma za ndani, na kutekeleza Kanuni za Hiyari za Usalama na Haki za Binadamu (VPSHR);
- Kuwezesha kujenga ushirikiano kwa faida ya Mradi na wadau ikiwa ni pamoja na Asasi za Kiraia na kudumisha heshima;
- Kubainisha mapema fursa na hatari zinazohusiana na shughuli ili kuingilia kati na kuepuka kuenea kwa tatizo pindi hatari ikijitokeza; na
- Kuhakikisha kuwa maswali ya wadau yanajibiwa kwa wakati kupipitia ushirikishaji endelevu.

Kanuni na Malengo ya Ushirikishaji

Mradi huu umejikita katika uwazi, majadiliano na ushirikishaji kwa sababu unategemea uhusiano wa muda mrefu na ulio wazi na wadau katika ngazi zote kama njia muhimu ya mafanikio yake. Katika Mfumo wake wa Ushirikishaji wa Wadau[9], Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki umeorodhesha kanuni na malengo yanayoongoza shughuli zake za ushirikishaji kwa kuzingatia viwango vya kimataifa, sheria za nchi na miongozo ya kampuni tanzu.

Wadau Wenye Maslahi na Walioathiriwa

Jedwali linalofuata linaeleza makundi tofauti ya wadau walioguswa yaliyobainishwa kulingana na shughuli za ushirikishaji za Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu. Katika makundi haya, kuna makundi madogo tofauti kama vile makundi yaliyo katika hali hatarishi ikiwa ni pamoja na makundi maalum kwenye jamii yaliyo katika hali hatarishi.

Jedwali ES-6: Muhtasari wa Wadau Walioguswa na Mradi na Athari za Kuhamisha Watu na Makazi

Kundi la Wadau	Athari zinazohusiana na Kuhamishwa zinaweza kuwa:	Mvuto katika Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu
Watu Walioguswa na Mradi: Kundi hili linaguswa moja kwa moja na utwaaji wa ardhi katika maeneo ya kipaumbele na linapaswa kuhamishwa kutokana na kuondolewa katika makazi yao na shughuli zao za kiuchumi. Kundi hili linaweza kujumuisha watu binafsi, kaya na vijiji ambavyo ardhi yake imeathiriwa. Kundi hili linapewa kipaumbele katika kushirikishwa. Watu hawa wanatambuliwa na kuwekwa katika kumbukumbu katika ukaguzi wa kina na shughuli za kutambua thamani zinazofanyika.	Kuondelewa katika makazi kutokana na kupoteza nyumba. Kuondolewa katika maeneo ya shughuli zao za kiuchumi kutokana na kupoteza ardhi/uwezekano wa kupata ardhi/rasilimali/uwezekano wa kupata rasilimali. Athari za kiuchumi kutokana na kupoteza maeneo ambayo ni sehemu shughuli zao za kuzalisha kipato (mf. mabwawa ya kuvua samaki) Athari za mahusiano ya kijamii na njia za kujikimu kutokana na mabadiliko katika kufikia jamii na njia za kuzalisha kipato.	Athari za mradi katika ardhi na nyumba za Walioguswa. Uhalali wa uthibitisho. Viwango na michakato ya fidia. Kubadili mali . Fursa za urejeshaji wa njia za kuzalisha kipato. Msaada wakati wa mchakato wa kuwahamisha watu. Ratiba na shughuli za ujenzi. Fursa za ajira Faida kwa jamii za mahali hapo..
Jamii Zilizoguswa na Mradi: Kundi hili linajumuisha jamii ambazo kwazo watu watahamishiwa na jamii wenyeji ambapo waathiriwa wa mradi watahamishiwa. Jamii hizi zimeelezwa zaidi katika Sura ya 5.	Utenganishaji wa Makazi (mf. jamii kugawanyika katika sehemu mbili kutokana na barabara) Mgawanyiko/migogoro ya kijamii (mf. utamaduni wa wanajamii wapya kutofautiana na wanajamii wenyeji).	Maendeleo ya Mradi. Mchakato wa uhamishaji. Ratiba na shughuli za ujenzi.. Fursa za ajira. Faida kwa jamii za mahali hapo..

Wadau Watakaovutiwa ni yale makundi ambayo hayaathiriwi moja kwa moja na utwaaji wa ardhi katika maeneo ya kipaumbele lakini, kwa nafasi yao, maarifa na/au uzoefu, yanaweza

[9] Mhimili wa Uhusishwaji wa Wadau wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki. Nyaraka Namba: UT-MID-60-0120-200055, Revision 00, 14-03- 2017.

kuathiri matokeo ya Mradi. Makundi haya yanajumuisha Serikali, Asasi za Kiraia, Asasi zisizo za Kiserikali, vyombo vya habari, na biashara/viwanda.

Muundo wa Ushirikishaji wa Mradi

Ushirikishaji wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki umebuniwa na unatekelezwa na timu za ushirikishaji za mradi kwa kushauriana na wadau muhimu wa Serikali ya Tanzania na wadau wa jamii. Timu hizi zinatumia miundo na michakato kadhaa kuhakikisha kuwa kunakuwa na mawasiliano sahihi na yenye tija ambayo yamebuniwa kukidhi mahitaji ya makundi mbalimbali ya wadau.

Mradi una timu tatu zinazohusika na ushirikishaji na mashauriano katika utwaaji na uhamishaji: timu ya mipango na utekelezaji wa Mpango Kazi wa Mradi wa Kuwahamisha Watu; timu ya ushirikishaji wa wadau wa Mradi; na timu ya mipango wa Mpango Kazi wa Mradi wa Kuwahamisha Watu ya Digby Wells Consortium (zikiwemo rasilimali za ushirikishaji wadau wa Mradi). Shughuli zote zinaongozwa na mfumo wa ushirikishaji wa wadau wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki na zinaratibiwa kwa kufuata mfumo huu.

Kikundi Kazi cha Ardhi na Uhamishaji wa Watu ni kamati inayoundwa na wawakilishi wa Mradi Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki na Serikali ya Tanzania. Ilianzishwa Machi 2018 katika hatua za mwanzo za mchakato wa kutwaa ardhi ya Mradi, na hukutana mara kwa mara ili kupokea taarifa mpya kuhusu utwaaji wa ardhi na mchakato wa kuhamisha watu, hujadili masuala na kutoa maoni kuwa mpango. Kamati hii inaongozwa na Mratibu wa Mradi kutoka Wizara ya Nishati. Timu ya masuala ya Ardhi na Kijamii ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki inatoa msaada wa masuala ya uhazili pamoja na mwakilishi wa Kikundi Kazi cha Ardhi na Uhamishaji wa Watu kutoka TPDC.

Njia za Ushirikishaji

Njia kadhaa za ushirikishaji zimetumika kusaidia ushirikishaji unaohusiana na mpango wa ujamishaji wa watu. Njia hizo zinajumuisha:

- Mikutano ya Kikundi Kazi cha Ardhi na Uhamishaji wa Watu na mikutano mingine ya Serikali/mikutano na idara maalum za serikali;
- Mikutano ya mara kwa mara katika ngazi ya mkoa na mikoa inayohusika na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki. Mikutano ya karibuni ya Ushirikishwaji ilifanyika mwezi Disemba mwaka 2018 na ilihusisha kuwekwa wazi kwa Mfumo wa Sera ya Kuwahamisha Watu kwa wadau wa mikoa na wilaya husika;
- Mikutano ya mara kwa mara na Wizara za serikali ili kujadiliana masuala yanayohusu uhamishaji wa watu na makazi; na
- Mikutano ya jamii/mikutano na vikundi maaalum iliyofanyika katika ngazi za wilaya, kata na kijiji. Hii ilijumuisha mikutano ya utoaji elimu; michakato ya upimaji; kuweka wazi taarifa za ardhi na mali zilizokusanywa wakati wa upimaji; uhakiki wa ardhi na mali; na kuweka wazi Majedwali ya Ulipaji wa Fidia. Zimetumika pia kama njia ya kukusanya data za maelezo kupitia majadiliano ya vikundi lengwa pamoja na mahojiano yasiyokuwa na mtiririko rasmi ili kuelewa vikwazo, changamoto na fursa za Watu watakaoguswa na Mradi katika sehemu za Maeneo Yaliyopewa Kipaumbele.

Mikutano hii imehuisha mikutano ya vikundi lengwa/vikundi vidogo pamoja na vikundi vidogo vya jamii vilivyokatika hali hatarishi.

Kuwekwa Wazi Mfumo wa Sera ya Uhamishaji Watu na Makazi na Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi katika Maeneo Yenye Kipaumbele

Masharti ya kimataifa yanatamka kuwa Mfumo wa Sera ya Mradi ya Uhamishaji Watu na Makazi na Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi katika Maeneo ya Kipaumbele vinapaswa kuwekwa wazi kwa umma. Mfumo wa Sera ya Uhamishaji wa Watu na Makazi umewekwa wazi kwa Umma na Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi katika Maeneo ya Kipaumbele unapatikana katika tovuti ya mradi katika lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili[10].

Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi katika Maeneo ya Kipaumbele ulikabidhiwa kwa Serikali ya Tanzania mnamo Desemba ili kuwa na muda wa siku 30 za kutoa maoni na imepangwa kuwa utawekwa wazi kwa umma kuanzia Machi 2019. Mambo ya msingi ya Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi yatatolewa muhtasari na kutafsiriwa katika lugha ya Kiswahili ili kupata muhtasari usio wa kitaalamu kwa ajili ya kuzipatia Kamati za Maendeleo za Kata na Kamati za Maendeleo za Vijiji na bango litatundikwa katika sehemu muhimu za makutano katika ngazi za serikali za mitaa (mf. katika ofisi za mikoa, wilaya na kata). Aidha toleo lililorahisishwa la Mfumo wa Stahiki ulioboreshwa uliomo katika Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi litatafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. Waraka huu utakabidhiwa kwa kila wilaya iliyoathiriwa na Mradi. Nakala za Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi (katika lugha ya Kiingereza) zitapatikana makao makuu ya mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki jijini Dar es Salaam, vituo vya Afisa Mahusiano Jamii mkoa (vitakapoanzishwa) na katika tovuti ya Mradi. Kijitabu kinachoonyesha kwa muhtasari mchakato unaoendelea kitasambazwa pamoja na muhtasari wa utendaji.

[10] Nyaraka maalum zinazopatikana katika tovuti ya Mradi ni: i) Waraka wote ya Mfumo wa Sera ya Kuwahamisha Watu iliyo katika lugha ya Kiingereza; na ii) Muhtasari wa waraka wa Mfumo wa Sera ya Kuwahamisha Watu ulio katika lugha ya Kiswahili (hii inajumuisha Muhtasari wa Kiutendaji na Sura ya 6 Mfumo wa Ustahili na Stahiki/Fidia).

10. MFUMO WA UTEKELEZAJI

Mfumo wa Kitaasisi

Kama ilivyoelezwa katika Mchakato wa Utwaaji wa Ardhi, awamu ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi utajumuisha mapendekezo kutoka Timu ya Mradi wa Bomba la Mafuta (PPT), pamoja na Serikali ya Tanzania. Majukumu na wajibu kwa awamu ya Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi katika Maeneo ya Kipaumbele yametolewa kwa muhtasari hapo chini.

Jedwali ES-7: Majukumu ya Kitaasisi katika Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi

Shughuli	Jukumu la Kampuni ya Mradi	Jukumu la Serikali ya Tanzania
Hatua ya 5: Kubadilisha Ardhi kuwa ya Matumizi ya Jumla na kwa Manufaa ya Umma	• Kutoa ramani na taarifa (pamoja na orodha ya vijiji vilivyoathiriwa) ya ardhi inayotakiwa kwa ajili ya Mradi kwa kila kipengele. • Kupitia eneo litakalotangazwa katika gazeti la serikali na amri nyinginezo na/au notisi kabla ya kuchapishwa katika gazeti la serikali.	• Kuandaa, kutoa na kuchapisha maagizo na/au notisi katika Gazeti la Serikali kama inavyotakiwa na Sheria ya utwaaji Ardhi. Serikali ya Tanzania itaandaa nyaraka kwa maandishi inayothibisha kuwa ardhi imetwaliwa kwa manufaa ya umma kwa ajili ya Mradi. • Kuchukua hatua na vitendo vyote muhimu ili kutimiza masharti ya Sheria ya Utwaaji wa Ardhi, ikiwa ni kwa ajili ya uchapishaji katika gazeti la serikali na utwaaji wa ardhi na kwa ajili ya kubadili matumizi ya ardhi fulani (kwa kuzingatia muda uliokubaliwa na Mradi) kuwa Ardhi ya Jumla kama ilivyokubaliwa kwa pamoja na Mradi[11].

[11] Hii inatarajiwa kujumuisha, bila kujifunga katika haya pekee: ithibati zote zinazohitajika kutoka katika mamlaka za Kijiji/Mtaa, Kata, Wilaya, Mikoa na Taifa; maazimio ya masuala yote ya mipango; upimaji na ripoti za lazima; notisi kama inavyoelezwa katika sheria na uchapaishaji wa notisi hizo, kama inavyotakiwa, katika Gazeti la Serikali. Tangazo la kutwaliwa kwa ardhi kwa ajili ya manufaa ya umma na kubadilishwa kutoka Ardhi ya Kijiji na ya Hifadhi hadi kuwa Ardhi ya Matumizi ya Jumla katika gazeti la serikali litokee mtawalia.

Shughuli	Jukumu la Kampuni ya Mradi	Jukumu la Serikali ya Tanzania
Hatua ya 6: Makubaliano ya Ulipaji wa Fidia	• Kutoa muda kwa serikali ya Tanzania na kukubali maelezo ya notisi ya dhamira ya kutwaa ardhi; • Kuongoza ushirikishaji wa Watu Walioguswa na jamii ili kufikia makubaliano ya ulipaji wa fidia; • Mradi kuwa sehemu ya makubaliano ya utoaji wa fidia na stahiki nyingine. Mradi utalipa fidia na kutoa stahiki za ziada chini ya viwango vya kimataifa; na • Kubaini masuala ambayo yatahitaji serikali ya Tanzania kutumia mamlaka ya utwaaji wa ardhi kwa lazima, na inapobidi, kuwezesha mchakato wa kutumia mamlaka hayo ya utwaaji huo wa lazima kwa kutoa taarifa stahiki.	• Kuandaa makubaliano na Kampuni inayoendesha Mradi, kutoa makubaliano hayo kwa wakati kama inavyoombwa na Kampuni ya Mradi na kuchapisha notisi ya dhamira ya kutwaa ardhi ya watu watakaoathiriwa (na vijiji vitakavyoathiriwa kama inavyotakiwa chini ya Sheria ya Utwaaji wa Ardhi); na • Kuwa sehemu ya utatu wa makubaliano ya ulipaji fidia. Serikali itakuwa Mamlaka ya Utwaaji wa ardhi
Hatua ya 7: Ulipaji wa Fidia, Uhamishaji na Utekelezaji wa Kurejesha Njia ya Kuzalisha Kipato na Programu za Msaada	• Kulipa fidia au stahiki nyinginezo na kurejesha njia za kuzalisha kipato na hatua za msaada; na • Kutoa muda na kukubali maneno ya notisi yalivyoandikwa ili kupata umiliki.	• Kuandaa makubaliano na Kampuni inayoendesha Mradi, kutoa makubaliano hayo kwa wakati kama inavyoombwa na Kampuni ya Mradi na kuchapisha notisi ya dhamira ya kutwaa ardhi ya watu watakaoguswa(na vijiji vitakavyoathiriwa kama inavyotakiwa chini ya Sheria ya Utwaaji wa Ardhi); na • Kusimamia ulipaji wa fidia na mchakato wa kuwahamisha watu.
Hatua ya 8: Haki ya Umiliki/Mamlaka iliyotolewa kwa Serikali ya Tanzania	Serikali itatekeleza hatua zote muhimu kuipatia mamlaka husika, ikiwa ni pamoja na, kama inavyofaa, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, “Haki ya Umiliki” wa ardhi iliyo katika eneo la kipaumbele (haki hiyo ya umiliki itaiwezesha Serikali kuupatia Mradi haki za ardhi zinazoendana na kanuni za Makubaliano ya Ushirikiano Baina ya Serikali Mbili (taz. Hatua ya 9)).	
Hatua ya 9: Ridhaa ya Kuukodishia Mradi Ardhi	Mamlaka husika (ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kwa ardhi iliyo katika Eneo la Kipaumbele) kuukodishia Mradi kwa kipindi kinachotakiwa (kwa maeneo ya kipaumbele, kwa kipindi cha miaka mitano ya mwanzo ama Mradi ueleze vinginevyo), ambayo inatoa haki ya ardhi kwa Mradi kama kanuni zinavyoeleza katika Makubaliano ya Ushirikiano Baina ya Serikali Mbili (na makubaliano mengine yaliyopo kwa kipindi hicho kati ya serikali Kampuni ya Mradi).	

Bajeti ya Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi

Bajeti ya kina kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Kuwahamisha Watu na Makazi imeandaliwa kwa kuzingatia umbali ulioripotiwa katika Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu katika Maeneo ya Kipaumbele na stahiki zilizoelezwa katika Sura ya 6 ya Mpango Kazi huu wa Kuwahamisha Watu. Vipengele vya bajeti kuu ni kama vifuatavyo:

- ***Ardhi- bei ya ardhi***, ya eneo la ardhi litakalochukuliwa na Mradi na viwango vya soko vya ardhi kama vilivyobainishwa katika makadirio yaliyofanywa kitaalamu. Katika kukadiria gharama ya ardhi, posho imewekwa kwa ardhi yatima. Gharama za miamala zimejumuishwa katika gharama ya ardhi;

- Wamiliki wa ***nyumba za kuishi*** zilizoathiriwa na Mradi watakuwa na haki ya kuchagua kati ya fidia ya fedha na kupatiwa nyumba badala yake itakayokuwa na ukubwa wa kutosha. Utekelezaji wa bajeti ya Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu Walioathiriwa umechukulia kuwa Watu wote Walioguswa na Mradi watachagua chaguo lenye gharama zaidi ambalo ni nyumba ya makazi badala ya fidia ya fedha. Fidia ya fedha kwa ***majengo madogo*** (kwa kuzingatia thamani ya kuhamishwa bila kuhusisha uchakavu) imejumuishwa katika bajeti ya utekelezaji;
- Fidia ya fedha kwa ***mazao na miti ya biashara*** imejumuishwa katika bajeti kwa kuzingatia kiasi cha uthaminishaji kilichoamuliwa wakati wa mapitio ya uthaminishaji wa mali;
- ***Posho*** mbalimbali zimejumuishwa ikiwa ni pamoja na posho ya usumbufu kwa kaya zilizoondolewa katika makazi na katika maeneo yao ya kiuchumi, na posho ya malazi na usafiri kwa watu walioondolewa katika makazi yao;
- Fidia iliyopangiwa bajeti kwa ajili ya ***uhamishaji wa makaburi*** inajumuisha gharama za kuhamisha makaburi yaliyoathiriwa na malipo ya fidia kwa ndugu yanayotakiwa chini ya mfumo wa kisheria;
- Bajeti kwa ajili ya hatua za kurejesha njia ya kuzalisha kipato inajumuisha mambo matatu makuu: i) gharama zinazohusiana na malazi ya muda mfupi, msaada kipindi cha mpito na/au hatua za kuhakikisha kunakuwa na chakula ili kuwalisha watu watakaohamishwa katika makazi yao na watakaohamishwa katika sehemu zao za uzalishaji wa kipato kabla ya ardhi ya fidia kupatikana; ii) Gharama zinazohusu hatua za urejeshaji wa njia za kuzalisha kipato za watu binafsi pamoja na kaya; na iii) gharama zinazohusiana na urejeshaji wa njia za kuzalisha kipato katika ngazi ya jamii au kijiji. Nyongeza ya bajeti imezingatia idadi ya vijiji vilivyoathiriwa na tathmini ya Maeneo ya Kipaumbele na athari katika ardhi ya jumuiya na sababu nyingine;
- Nyongeza imewekwa kwenye bajeti kwa ajili ya msaada wa ziada kwa ***watu na/au kaya zilizo katika mazingira magumu***; na
- Bajeti ya rasilimali zinazohitajika katika ***utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi.***

Programu ya Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi kwa ajili ya Awamu ya Utekelezaji

Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu unawasilisha ratiba ya hali ya juu kwa ajili ya Awamu ya Kupanga Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na kuangalia Awamu ya Utekelezaji.

Ili kumwezesha mkandarasi kutumia ardhi ya maeneo ya kipaumbele, malazi ya muda yatapangwa kwa ajili ya Waguswa watakaohamishwa makazi , pamoja na msaada wa ziada wa kujikimu kati ya wakati wa Waguswa kutia saini makubaliano ya kuhama/kupokea malipo na hatua ya kuhamia katika makazi mapya au ardhi mpya. Ratiba ya utekelezaji kwa maeneo ya kipaumbele imezingatia kuwa uwezekano wa kufikia maeneo ya Eneo la Kufunikia Bomba la Mafuta Ghafi ili liweze Kutunza Joto -KP701, KAMBI KUU-08 na KAMBI KUU-16 bado ni

ngumu kwa Mradi kwa sababu malipo ya fidia kwa maeneo ya kipaumbele yamepangwa kuanza Machi 2019.

Wakati wa mikutano zaidi ya kuelimisha jamii, taarifa kuhusu stahiki za Watu walioguswa na mradi, taarifa za wakati huo za ushirikishaji wa Afisa Mahusiano katika Jamii wa Mradi unaondelea zitatolewa kwa Waguswa na wadau husika katika ratiba ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kuwahamisha Watu.

UFUATILIAJI NA TATHMINI

Ufuatiliaji wa aina kuu nne utafanyika:

- **Ufuatiliaji wa mchakato**, ni shughuli ya ufuatiliaji wa ndani wenye lengo la kufuatilia athari za mchakato wa utekelezaji wa uhamishaji wa Watu walioguswa na zoezi hilo, kwa kaya zao na jamii zilizowapokea. Viashiria vya zoezi hili vinajumuisha ushauri uliokamilika na unaoendelea, malalamiko yaliyoibuliwa na kushughulikiwa, malipo ya fidia yaliyotolewa, n.k. Ufuatiliaji huo unawezesha kuwa na utekelezaji unaozingatia wakati wa hatua za pamoja pale inapohitajika. Inashauriwa ufuatiliaji wa ndani uwe unafanyika kila baada ya miezi 3 wakati wa utekelezaji;
- **Ufuatiliaji wa iwapo Masharti Yamezingatiwa**, ambao unalenga kuthibitisha iwapo utekelezaji wa kuhamisha watu na makazi unakidhi malengo ya msingi kama yalivyofafanuliwa katika Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi/Mpango wa Kurejesha Njia za Kuzalisha Kipato:na kwamba Watu walioguswa na Mradi wamepokea fidia stahiki zinazoendana na mfumo stahiki; na kwamba wanaweza kurudia njia zao za kujikimu kimaisha baada ya kuhamishwa. Njia za ufuatiliaji zitajumuisha upimaji wa kijamii na kiuchumi wa mara kwa mara (ili kulinganisha mabadiliko katika sifa ya kaya kwa kuwianisha na hali ya mwanzoni iliyotolewa taarifa katika Sura ya 5) na ufuatiliaji wa ushiriki unaohusisha mashauriano na wadau ili kupata mapendekezo na maoni yao. Ufuatiliaji wa kufuata masharti unapaswa ufanyike wakati wa utekelezaji na kwa muda wa miaka miwili baada ya watu kuhamishwa, na baada ya hapo utakuwa ukifanyika mara mbili kwa mwaka;
- **Ukaguzi wa ukamilifu,** baada ya kukamilika kwa utekelezaji wa mpango wa kuwahamisha watu/kuwarejeshea njia za kuzalisha kipato. Ukaguzi huu utafanywa na mkaguzi huru na mwenye sifa kutoka nje atakayetafutwa na Kampuni inayohusika na Mradi kwa kushirikiana na wadau. Lengo kuu la ukaguzi wa ukamilifu ni kuthibitisha iwapo Watu walioguswa na Mradi wameweza kurejesha njia zao za kuingiza kipato au iwapo kuna hatua za kuboresha zinazopaswa zichukuliwe. Viashiria vitakavyotathminiwa vinajumuisha mabadiliko ya mikakati ya kuingiza kipato na vyanzo vya mapato, mabadiliko katika hali za kaya zilizo katika mazingira magumu, mabadiliko katika mazao ya kilimo na kipato kitokanacho na kilimo, n.k.; na
- **Tathmini baada ya Mradi Kukamilika**, itafanywa na mtaalamu huru na mwenye sifa, baada ya miaka mitatu hadi mitano ya utekelezaji wa kuwahamisha watu. Lengo la tathmini hii ni kupima athari za muda mrefu ambazo zimetokana na uhamishaji wa watu kwa Walioguswa na mradi na kwa jamii zilizowapokea, na iwapo ulipaji wa fidia

na urejeshaji wa njia za kuingiza kipato umeleta manufaa yaliyotarajiwa katika namna endelevu.

Kampuni inayohusika na Mradi itakuwa na wajibu wa kutoa rasilimali watu, mafunzo, fedha na vifaa kwa ajili ya utekelezaji wa programu ya ufuatiliaji pamoja na tathmini yoyote kutoka nje. Programu za ufuatiliaji zitaundwa na kutekelezwa na Timu ya Wataalamu kwa kushirikiana na watu waliothiriwa na mradi pamoja na wadau wengine.

KIAMBATISHO 1.

6. VIGEZO, STAHIKI NA CHAGUZI ZA FIDIA

6.1. Mfumo wa Stahiki

Jedwali 6-1 linaorodhesha aina mbalimbali za stahiki zilizofafanuliwa katika mfumo wa stahiki uliowekwa kwenye Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi. Jedwali hili linajumuisha aina zinazotumika katika Maeneo ya Kipaumbele tu. Hivyo, kwa mfano, Stahiki ya kipengele D (kupoteza majengo rasmi ya biashara) haikujumuishwa katika Jedwali 6-1 kwa kuwa hakuna majengo maalum ya biashara yaliyoathiriwa na Maeneo ya Kipaumbele. Namba za aina stahiki zilizoainishwa katika Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi zilibakizwa.

Jedwali lifuatalo la 6-1 linaonyesha kwa kina zaidi kuhusu fidia na stahiki za msaada chini ya masharti ya nchini Tanzania na ya kimataifa ya ukopeshwaji.

Jedwali 6-1: Muundo wa Stahiki – Maeneo ya Kipaumbele

Athari		Madhara	Wenye Stahiki	Stahiki
Ardhi	A1 Kupoteza Ardhi na makazi – kiwanja chote kimechukuliwa (kwa sababu chote kinaangukia[1] kwenye eneo la Mradi au kwa sababu ardhi iliyobaki imechukuliwa kama ardhi yatima na athari za jumla ya kuchukua ardhi yote ya mguswa kunaweza kuathiri uwezo wao wa kujikimu kimaisha)	Ardhi inatwaliwa moja kwa moja	Kaya itapoteza moja kwa moja au kushindwa kutumia nyumba zao za makazi	***Chaguo la mali kwa mali 1:*** • Kupewa ardhi mbadala inayolingana ukubwa na ardhi iliyochukuliwa, mahali panapofaa yenye usalama wa milki kulingana na vigezo vya utekelezaji vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC)PS5; • Malipo ya gharama zote za miamala[2]; • Posho ya Usumbufu;[3] • Posho nyingine kama zinavyostahili; na • Ushiriki katika programu a shughuli za kurejesha kipato (Kundi 1).[4] [5] ***Chaguo la Mali kwa mali 2:*** • Kupatiwa ardhi/ kiwanja mbadala cha makazi mahali panapofaa, kikiwa na usalama wa milki kulingana na vigezo vya utekelezaji vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC) PS5 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba mbadala (iwapo anastahili chini ya B1 / B2 na chaguo la nyumba mbadala limefanywa na mguswa); • Fidia ya fedha taslimu kwa ajili ya ardhi ya mguswa iliyotwaliwa ambapo ardhi mbadala hajapewa (iwapo anastahiki); • Mradi unasaidia kutafuta ardhi ya kubadili sehemu iliyofidiwa fedha taslimu; • Posho ya usumbufu; • Posho nyingine kama zitakavyoonekana; na • Ushiriki katika programu ya shughuli za kurejesha kipato (Kundi 1)

[1] Nyumba za makazi zipo katika ardhi iliyoathiriwa ndani ya eneo la Mradi au katika ardhi inayochukuliwa kuwa yatima. Watu Walioguswa na Mradi wanaweza kuwa na shamba la ziada/ardhi nyingine nje ya eneo la Mradi ambayo bado inachukuliwa kuwa inafaa.
[2] Kwa ajili ya gharama za muamala au usajili gharama halisi itajulikana kutoka mamlaka ya serikali za mitaa.
[3] Kama ilivyoonyeshwa Posho ya Usumbufu ilifafanuliwa kama kiwango cha wastani wa asilimia ya riba inayotolewa na benki za biashara katika akiba za muda maalum kwa miezi kumi na miwili wakati wa kupoteza riba katika ardhi (tazama Ibara 6.2.4 ya Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi katika Maeneo ya Kipaumbele – PA RAP).
[4] Programu hizo zitachimbuka kutokana na matokeo ya utafiti wa kijamii na kiuchumi na sensa kuunda sehemu ya mchakato wa Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi / Mpango wa kuwarejeshea watu njia za uzalishaji kipato.
[5] Stahiki ya Watu walioguswa na Mradi kushiriki katika programu za kuzalisha kipato ambapo sehemu ya kiwanja iliyochukuliwa bado inafaa kutumika katika Maeneo ya Kipaumbele. Vigezo vya kustahiki bado havijakamilika na vinaweza kutofautiana.

Athari		Madhara	Wenye Stahiki	Stahiki
				AU **Chaguo la Fedha Taslimu**: • Fidia (iwapo anastahili) ya ardhi aliyopoteza moja kwa moja kwa viwango vya soko kama vilivyofafanuliwa na Mthamini Aliyesajiliwa;[6] [7] • Posho kama hapo juu; na • Ushiriki katika programu ya shughuli za kurejesha kipato (Kundi 1).
	A 3 Kupoteza moja kwa moja ardhi yote ya kilimo (mazao) ambapo kiwanja kilichopo kimeathiriwa au sehemu iliyobaki haifai (ardhi yatima na athari ya umiliki wa ardhi wa mguswa inauwezekano wa kuathiri kwa kiasi kikubwa shughuli za uzalishaji kipato	Ardhi inatwaliwa moja kwa moja	Mmiliki wa ardhi kisheria[8] / Mmiliki wa ardhi kimila **na** Kaya itapoteza ardhi, mazao na / au miti, na inachukuliwa kuwa katika hali hatarishi kulingana na vigezo vilivyoonyeshwa hapo chini, ikiwa ni pamoja na kutegemea kilimo kama shughuli ya msingi ya kuingiza kipato na jumla ya ukubwa wa ardhi inayomilikiwa na kaya (nje ya eneo la Mradi), baada ya kuondolewa, ni sawa na au pungufu ya ekari 2.5.	• Sawa na stahiki za A1 kwa kuwa athari zinafanana (tazama hapo juu); • Ushiriki katika programu ya shughuli za kurejesha kipato (Kundi 1/2)
	A 4 Kupoteza moja kwa moja sehemu ya ardhi ya kilimo (mazao) na sehemu inayobaki (au jumla ya ardhi yote anayobaki nayo mguswa) inaweza kuendelea kusaidia shughuli zake za kuingiza kipato[9] au iwapo matumizi ya awali ya ardhi yataendelea baada ya ujenzi kukamilika).	Ardhi kutraliwa moja kwa moja	Mmiliki wa ardhi kisheria Mmiliki wa ardhi kimila	• Fidia (iwapo anastahili) kwa ardhi iliyotwaliwa moja kwa moja kwa viwango vya soko kama vilivyofafanuliwa na Mthamini Aliyesajiliwa (pamoja na gharama za miamala yote); • Posho zinazostahili; na • Ushiriki katika programu ya shughuli za kurejesha kipato (Kikundi 2).

[6] Inapowezekana, dhamana inaweza kukatwa kutoka katika malipo yanayolipwa na kulipwa kwa taasisi inayokopesha. Kanuni hii inatumika kwa mali zote ambazo zimezuiwa na dhamana.
[7] Viwango vya soko vilivyoelezwa na Mthamini aliyesajiliwa vinawasilishwa kwa Mthamini Mkuu (MLHHSD) ili kupata ithibati. Viwango vya ardhi vilivyothibitishwa ndivyo vitakavyotumika katika uthaminishaji.
[8] Kwa waguswa wa mradi hii inajumuisha wamiliki wa kitaasisi wa ardhi ya Hifadhi katika MCPY-07 ambayo ni kwa ajili ya elimu na inatumiwa na wafanyakazi kutoka shuleni kwa ajili ya kilimo.
[9] Inachukulia kuwa Programu ya Shughuli za Kurejesha Kipato ipo tayari..

Athari		Madhara	Wenye Stahiki	Stahiki
	A 5 Kupoteza moja kwa moja ardhi ya kilimo (mazao)	Ardhi inatwaliwa moja kwa moja	Watumiaji ardhi wanaotambulika ila si wamiliki rasmi (pamoja na wapangaji wakazi)[10] Watu wenye milki zisizo rasmi[11]	• Hakuna kwa anayepoteza ardhi. Rejea katika vipengele B na I husika hapo chini kuhusu stahiki kwa kupoteza mali[12]. • Mradi unaweza pale watu wenye umiliki usio rasmi na pia wanatambulika kuwa katika hali hatarishi, kuwapatia ardhi mbadala yenye usalama wa milki (kila mguswa atashughulikiwa kutegemea na hali yake).
	A 6 Kupoteza moja kwa moja ardhi ya malisho ya wanyama	Ardhi inatwaliwa moja kwa moja	Mmiliki wa ardhi kisheria Mmiliki wa ardhi kimila	• Fidia ya fedha taslimu ya thamani ya ardhi kwa gharama zote kamili za ununuzi kwa thamani ya bei ya soko kama iliyoelezwa na Mthamini aliyesajiliwa pamoja na gharama zingine); na • Stahiki nyingine ikiwa ni pamoja na posho ya usumbufu, posho zingine zinazohusika; na ushiriki katika programu ya shughuli husika ya kurejesha kipato.
	A 7 Kupoteza moja kwa moja ardhi isiyolimwa/ardhi tupu[13]	Ardhi inatwaliwa moja kwa moja	Mmiliki wa ardhi kisheria Mmiliki wa ardhi kimila	• Fidia ya fedha taslimu kwa ajili ya ardhi isiyolimwa/ardhi tupu kwa thamani ya sokokama iliyoelezwa na Mthamini Aliyesajiliwa (pamoja na gharama za miamala).

[10] Hii inahusu ardhi inayomilikiwa au kuhodhiwa na mtu binafsi na kupangishwa kwa upande wa tatu. Wapangaji wanatambuliwa kwa kuwa wana maslahi, lakini hawana umiliki wa ardhi chini ya Kanuni za Uthamini na Usajili wa Wathamini (Jumla), 2018. Kwa ardhi inayohodhiwa na kutumiwa kijamii tazama H5 na H6.

[11] Wamiliki wasio rasmi wako kwenye mali ambayo inachukuliwa kuwa ya kudumu au kudumu kiasi na kuzuia maslahi mengine ya kishindani.

[12] Katika hali tofauti tofauti mradi ulichunguza kama mtu yoyote anayepanga au mkazi asiye rasmi katika Maeneo ya Kipaumbele na pia kutokana na ugumu wa mazingira waliyomo na mali walizopoteza kutokana na Mradi watastahili kupatiwa ardhi mbadala. Hakuna matukio kama haya yaliyobainishwa katika maeneo ya kipaumbele isipokuwa wapangaji watatu (waliokubaliwa na wenye nyumba wao) ambao wamepoteza nyumba zao za kuishi za kudumu (wanazo zimiliki) na wataondolewa katika maeneo hayo.

[13] Ardhi tupu ina maana ardhi ambayo inayoshikiliwa na inatumiwa (kulima), hata kama haitumiki wakati wa ukaguzi, lakini haijumuishi ardhi iliyotelekezwa.

Athari		Madhara	Wenye Stahiki	Stahiki
Mmiliki kupoteza Makazi[14]	B 1 Kupoteza nyumba kuu na nyumba nyingine za ziada zinazotumiwa na wenza au wanafamilia (kutegemea vigezo) – nyumba hizo lazima ziwe zinatumiwa na watu wakati ukaguzi unapo fanyika.[15]	Kupoteza nyumba yote au sehemu ya nyumba ambapo sehemu iliyobaki inakua haifai tena watu kuishi	Kaya itapoteza nyumba yake na nyumba zingine za ziada (au itapoteza njia za kuzifikia nyumba hizo) ambazo inazimiliki[16] (Hii inahusisha nyumba za makazi zilizokamilika tu).	**Chaguo la mali kwa mali:** • Wamiliki wa nyumba watapata nyumba mbadala na nyumba ndogo za makazi zenye muundo sanifu wa nyumba za kuishi. Mchoro/Muundo wa nyumba utafuata kanuni na viwango vya Tanzania na kuwa za viwango sawa au vinavyotosheleza kuliko nyumba zilizopo na kufuata viwango vyote vya ujenzi na mipango miji; • Malazi ya muda yatatolewa kuongezea msaada uliotolewa katika kipindi cha mpito (iwapo utahitajika wakati nyumba mbadala zinapojengwa) pamoja na malipo ya gharama za pango kwa ajili ya makazi ya muda zitatolewa na Mradi;[17] • Gharama za Miamala; • Gharama za usafirishaji kwa ajili ya kuondoa bidhaa za kaya na mali zingine zinazoweza kurudia kutumiwa na vifaa vya ujenzi vinavyoweza kusafirishwa kwenda makazi mbadala; • Posho ya Usumbufu; • Posho nyingine zinazohusika (yaani posho ya malazi na usafiri);[18] na • Ushiriki katika programu ya shughuli za za kuboresha uzalishaji wa mali.. AU • • Gharama kamili na timilifu ya kujenga nyumba kwa ujumla [19] • Nyumba Mbadala kwa ujumla; • Pale inapofaa, dhamana/mkopo utakatwa kutoka kwenye malipo yanayotolewa na kulipwa taasisi iliyokopesha[20]; • Posho ya Usumbufu; • Posho zingine kama inavyofaa (yaani posho ya malazi na posho ya usafiri) [21]; na • Ushiriki katika programu za kuboresha shughuli za kuzalisha kipato (yaani Kikundi..)

[14] Watu Walioguswa na Mradi Wenye Stahiki wataruhusiwa kuondoa vifaa vya ujenzi na vinginevyo ambavyo sio vya kudumu katika nyumba wanazo hama kabla ya kupewa makazi ya kuhamia.

[15] Nyumba za makazi za ziada na majengo mengine ya makazi yanayohamishika yatatathminiwa kwa kuzingatia sababu ya matumizi, mahali na kitamaduni.

[16] Kwa maeneo ya kipaumbele hii inajumuisha wapangaji watatu ambao **wanamiliki** n**a kukaa katika nyumba zilizoathiriwa** wakati wa uthamini.

[17] Hii inajumuisha wapangaji watatu ambao **wanamiliki** n**a kukaa katika nyumba zilizoathiriwa** wakati wa uthamini.

[18] Posho zingine zitajumuisha kiasi kinachochukuliwa kuwa kinatosha kuwezesha usafiri kwenda benki au taasisi zingine husika ili Watu Walioguswa na Mradi waweze kupata fedha zilizolipwa. Hii itakokotolewa kwa kuzingatia mkoa na mkoa na huenda katika ngazi ndogo ya mradi na itazingatia gharama za safari ya kwenda na kurudi kwa kutumia usafiri wa umma.

[19] Chaguo la fedha taslimu lipo kwa wamiliki wa nyumba wenye uthibitisho wa nyumba mbadala kwa ajili ya wanakaya waliobainishwa wakati wa sensa ya ukaguzi.

[20] Katika hatua ya kupanga Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi hakuna dhamana iliyobainishwa katika nyumba zote za makazi zilizoathiriwa.

Athari		Madhara	Wenye Stahiki	Stahiki
	B 2 Kupoteza makazi ya ziada (nyumba za kupangisha, malazi ya bure kwa ajili ya ndugu, n.k.)	Kupoteza nyumba yote au sehemu ya nyumba ambapo sehemu inayobaki haifai tena watu kuishi	Kaya itapoteza nyumba yake yote na nyumba zingine husika (au inapoteza njia ya kufika kwenye nyumba hizi) (Hii inahushisha nyumba zilizokamilika tu).	Kutegemea vigezo sawa na B1 na iwapo inafuata: **[Chaguo la Fedha Taslimu]** • Gharama kamili na timilifu ya nyumba kama ya nyumba kama ilivyokaguliwa; • Posho ya Usumbufu; na • Posho nyingine zinazohusika. AU **[Chaguo la Mali kwa Mali]** • Nyumba mbadala na majengo ya ziada ya kuishi yaliyotokana na mchoro sanifu wa nyumba. Mchoro/Muundo wa nyumba kwa kiwango cha ujumla utafuata kanuni na viwango vya Tanzania na utakua wa kiwango sawa au cha ziada kuliko nyumba zilizopo na kufuata viwango vyote husika vya ujenzi na mipango miji; • Malazi ya muda mfupi yatatolewa kuongezea katika msaada uliotolewa kipindi cha mpito (kama ikihitajika wakati nyumba mbadala inapojengwa) pamoja na malipo ya gharama za pango kwa ajili ya malazi ya muda yatakayotolewa na Mradi, na • Ushiriki katika programu ya shughuli za kuboresha njia za kuzalisha kipato. Posho: • Gharama za Miamala; • Gharama za usafiri kwa ajili ya kuondoa mali za familia na mali zingine zinazoweza kurudia kutumiwa na vifaa vya ujenzi vinavyoweza kusafirishwa kwenda makazi mbadala; • Posho ya Usumbufu; na • Posho zingine kama zinavyohusika. Vivutio: • Mradi unaweza kutoa kivutio cha kulipa fedha taslimu iwapo nyumba hizo mbadala zinazopaswa kujengwa zinaweza kujengwa ndani ya eneo lililopo la familia.
	B 3 Majengo ya ziada na nyumba ndogo, mazizi ya mifugo, visima,, mifumo ya maji taka ya vyoo, , maghala, uzio, ngazi za majengo, baraza za nyumba, njia zisizo za lami za kuingia nyumbani na mambo kama hayo – pamoja na majengo ambayo	Kupoteza Kabisa Majengo Mengine na Majengo ya Ziada	Mmiliki wa majengo – kumbuka kuwa hii inaweza isiwe sawa na mmiliki wa kiwwanja.	• Gharama za kubadili jengo hilo, kama halifai tena; • Majengo yasiyokamilika yatathaminiwa kwa Gharama za Kubadili kwa kuzingatia kiwango cha ukamilifu wa majengo; • Posho ya Usumbufu; na • Gharama za usafirishaji kwa ajili ya kuondoa bidhaa za kaya na vitu vinavyoweza kurudia kutumiwa na vifaa vya ujenzi vinavyoweza kusafirishwa kwenda eneo mbadala;

[21] Kaya zinazolima zaidi ya hekta moja ya ardhi walikuwa na matumizi ya chakula ya kiwango cha pointi 2.4 juu zaidi kwa wastani kuliko zile ambazo zililima chini ya hekta moja (ekari 2.5). – Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) Uchambuzi na Utambuzi wa Hali Hatarishi (VAM), 2010. Jamhuri ya Muungano ya Tanzania 2009/10 Uchambuzi Kabambe wa Usalama wa Chakula na Hali Hatarishi (CFSVA).

Athari		Madhara	Wenye Stahiki	Stahiki
	hayajakamilika			•
	B 4 Miundombinu ya usafi wa Mazingira	Kupoteza miundombinu ya usafi wa Mazingiwa	Wamiliki wa majengo ya makazi, biashara na majengo mengine. Wakala wa Serikali kama wamiliki wa miundombinu ya jamii.	• Gharama za nyumba/jengo mbadala; • Posho ya Usumbufu; na • Posho zingine kama zinavyohusika. na • Pale tu mtu anapopoteza nyumba za kuishi na anastahiki chini ya kipengele B1 na B2– Utoaji wa choo cha kisasa kulingana na vigezo vya stahiki ya nyumba (tazama Sehemu 6.4 ya Mpango Kazi wa Uhamishajiwa Watu na Makazi katika Maeneo ya Kipaumbele).
Kupoteza nyumba au ardhi inayomilikiwa na Jamii au Taasisi	H 4 Ardhi iliyotumiwa kwa madhumuni ya jamii, hususan ardhi ya malisho ya mifugo inayotumiwa kulishia mifugo mifugo kwa pamoja	Kupoteza Kabisa	Inamilikiwa na jamii[22]	• Fedha taslimu kwa ardhi iliyochukuliwa moja kwa moja thamani inategemea viwango vya soko na fidia inalipwa kwa jamii ya wafugaji (chombo kuteuliwa na jamii) au iwapo ni Ardhi ya Kijiji kwenda Halmashauri ya Kijiji; • Posho kama zinavyohusika. • (Maeneo ya waguswa yatazungushiwa uzio).
	H 5 Ardhi iliyotumiwa kwa ajili ya jamii, hususan ardhi ya malisho ya mifugo iliyotumiwa kwa ajili ya kulishia mifugo kwa pamoja	Kukosa njia ya kuingia kwa muda	Inamilikiwa na jamii	• Msaada wa Mradi katika kurekebisha njia ya kuingia au mipango mbadala wakati wa kipindi cha ujenzi. • (Maeneo ya waguswa yatazungushiwa uzio).
	H 6 Barabara, njia za waenda kwa miguu, mifereji na miundombinu ya umeme	Kupoteza kabisa miundombinu	Serikali ya wilaya na serikali ya mitaa, jamii, au kampuni ya huduma za umma.	• Kutoa barabara ndani ya jamii kwa viwango vya kitaifa vya usalama wa barabara ikiwa ni pamoja na mifereji na vivuko salama pale vinapohitajika; • Uchepushaji wa huduma na miundombinu kwa kufuata viwango vya kitaifa; • Kutoa barabara ya kufika kwenye maeneo wanayohamia iwapo hakuna barabara ya kuingia; na • Kubadili njia ya waenda kwa miguu kuzunguka miundombinu ya mradi kwa kuzingatia tathmini ya njia waliyopoteza.
Miti na Mazao	I 1 Kupoteza mazao ya msimu/miche iliyohamishwa na kupandwa baada ya kuvunwa	Kupoteza kabisa au kuzuiwa kuingia	Watu wote Walioguswa na mradi ambao wamepoteza mazao na miti yenye faida kiuchumi kama ilivyorekodiwa katika maeneo yao siku ya uthaminishaji (yaani walikuwepo wakati wa uthamini).	• Fidia ya fedha taslimu kulingana na kiwango cha ukomavu katika tarehe ya uthaminishaji. Kulingana na Viwango vya Utendaji kimataifa viwango vya mazao na miti vimerekebishwa kuakisi thamani ya soko kwa mwaka wa uthaminishaji 2018 (tazama Sehemu 6.3.1 ya Maeneo ya Vipaumbele Sera ya Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na
	I 2 Kupoteza mazao ya mwaka			
	I 3 Kupoteza mazao – ya msimu (mwaka)			

[22] Tazama rejea namba 9 na Maeneo ya Kipaumbele cha Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi Sura ya 5 (MCPY-07). Kufuatia mashauriano wakati wa kupanga mipango ya Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi kwa taasisi inayomiliki ardhi hii iliyoathiriwa itastahiki chini ya A3.

Athari		Madhara	Wenye Stahiki	Stahiki
	I 4 Kupoteza miti ya matunda yenye thamani kiuchumi ikiwa ni pamoja na miti ya matunda na mbao			Makazi katika Maeneo ya Kipaumbele).
	I 5 Kupoteza miti ya mbao yenye thamani kiuchumi			
	I 6 Kupoteza miti ya matunda au ya mbao			
	I 7 Kupoteza mali za kilimo			
Mali za Kitamaduni	J 2 Makaburi	Moja kwa Moja	Mtu au vikundi vinavyotoa madai ya makaburi	• Kuhamisha au kufungia kaburi kwa kushauriana na mdai au wawakilishi. Mradi umeanzisha Utaratibu wa Kuhamisha Makaburi.. Utaratibu huu utafuata masharti husika ya kisheria.); na • Mradi utatoa viwango vya fidia kwa ajili ya makaburi (kulingana na masharti ya kisheria) kwa kuzingatia maoni ya Mthamini aliyesajiliwa (kwa kuzingatia gharama za ujenzi, aina ya vifaa, gharama za uchimbaji, gharama za ibada ya mazishi) na Mwongozo wa Mthamini Mkuu wa Serikali kuhusu viwango vya kitaifa vilivyowekwa kwa aina za makaburi. Kwa ajili ya waguswa kiasi kisichozidi Shilingi za Kitanzania 500,000 kimeamuliwa kutumika.

Athari		Madhara	Wenye Stahiki	Stahiki
Watu au Vikundi Vilivyo katika hali hatarishi	K 1 Programu ya ziada ya msaada wa kijamii kwa watu walio katika hali hatarishi wanastahili manufaa yoyote kati ya hayo hapo juu	Kupoteza kwa Muda au Kabisa	Kaya ambazo zimehamishwa kimakazi au kiuchumi na Mradi. Kaya itachukuliwa kuwa na uwezekano wa kuwa katika hali hatarishi [23] iwapo angalau moja ya vigezo vifuatavyo vinahusika katika kaya: • Kaya inaongozwa na mwanamke; • Kaya inaongozwa na mzee (miaka 60 na zaidi); • Shughuli ya msingi ya kuingiza kipato kwa kaya ni kilimo, kaya itapoteza ardhi itakayoenda kwenye Mradi na jumla ya ukubwa wa ardhi ya kilimo inayomiliki baada ya kuondolewa ni sawa au pungufu ya ekari 2.5; na / au • Kaya ina mwanakaya mmoja au zaidi mwenye ulemavu wa viungo na /au akili. .	• Msaada ulioandaliwa kama ilivyotathminiwa kulingana na tukio ili kuhakikisha kuwa watu walio katika hali hatarishi wanapata fidia iliyokusudiwa na ulinzi kwa masharti ya Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi; • Msaada wa kisheria, kifedha na vitendo kama ilivyoamuliwa kutumika kwa kuzingatia tukio; na • Ushiriki katika programu za kuboresha njia za kuingiza kipato/kuzalisha mali.
Mpito wa Kifedha	L 1 Kupungua fedha taslimu	Kushindwa kwa kaya kumudu kupungua ghafla kwa fedha taslimu na kutenga kimakosa fedha kwa vitu vingine tofauti na vilivyokusudiwa.	Watu wote wanaopata fidia ya fedha taslimu zilizobainishwa kupitia sensa ya ukaguzi wa mwisho	• Mafunzo ya usimamizi wa fedha yatatolewa (ambayo yatakuwa yanahusiana na kiasi cha fidia ya fedha taslimu); na • Msaada wa kufungua akaunti za benki[24].

[23] Tazama sehemu 4.3 ya Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi katika Maeneo ya Kipaumbele (PA RAP).

[24] Kwa malipo ya fidia ndogo sana Mradi unatathmini njia zingine za malipo kwa ajili ya kutoa kwa usalama fedha hizo kwa Waguswa wa Mradi. Hizi zitajumuisha Waguswa ambao jumla ya malipo ya fidia yao ni chini ya Shilingi za Kitanzania 100,000. Hata hivyo, kiasi kidogo kwa malipo ya 'fidia ndogo sana' kitategemea uchanganuzi unaoendelea na majadiliano na wadau wa benki.

EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

EACOP PROJECT IN TANZANIA
TEAM – Total East Africa Midstream,
369 Toure Drive, Ground Floor, Kilwa House, Oysterbay,
P.O. Box 23917, Kinondoni, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: 0800 780 068 (Toll free) or +255 (0) 222 296 742
Email: EACOP.info@total.com
www.eacop.com

EACOP PROJECT IN UGANDA
TEAM - Total East Africa Midstream,
Plot 21, Yusuf Lule Road,
P.O.Box 34867, Kampala – Uganda
Tel: 0800 216 000 (Toll free) or +256 (0) 204 916 000
Email: EACOP.info@total.com
www.eacop.com

©EACOP. All rights reserved, March 2019